# *Mungu Anayo Njia Iliyoandaliwa*

Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo sasa, kabla hatujaomba. Je, kuna mtu yeyote aliye na haja maalum, usiku wa leo, ambalo ungependa Mungu akujibie? Inua tu mkono wako. Sasa, moyoni mwako wazia kile unachoomba. Vema. Na hapa kuna haja mbili hapa. Sasa, na tuinamishe vichwa vyetu.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia Kiti Chako cha neema. Kamwe tusingejaribu kuja kwa njia nyingine yoyote, kwa maana neema ndiyo tunayohitaji, Bwana. Hatungeweza kusimama kwenye Kiti cha Enzi cha hukumu, Yesu alisimama pale kwa ajili yetu. Na sasa tunasimama kwenye Kiti cha Enzi cha neema Yake pamoja na ahadi hii iliyobarikiwa kwamba tukiomba lolote kwa Jina Lake, tutapewa. Sisi ni watu wenye majaliwa sana, usiku wa leo, kuwa na ahadi hii.

3 Na, Baba, uliiona hiyo mikono, nami nina hakika unajua kilichokuwa chini yake, shauku ya moyo. Jibu, Bwana, sawasawa na utajiri Wako Utukufuni.

4 Ninauombea huu mkutano, kwa ajili ya mwenye dhambi, asiyeamini, mwovu; tunawaombea wagonjwa na wanaoteseka, hapa na kila mahali pia; kwa ajili ya ndugu wahudumu kote nchini, ambao wanashikilia taratibu za thamani za Bwana Yesu na Neno Lake. Utupe kumwagwa kukuu kwa Roho Wake, usiku wa leo, Bwana, juu yetu, ili tutakapoondoka, tuweze kusema, kama wale waliotoka Emau usiku ule, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akizungumza nasi njiani?” Tunaomba haya katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

Mwaweza kuketi.

5 Ni vema kuwa hapa tena usiku wa leo, katika dakika chache zilizopita nimepata fursa ya kupeana mikono na marafiki wa zamani, wahudumu ambao nimewajua nyakati za nyuma, Ndugu Andrew Rasmussen, mmoja wao, na mwingine alikuwa Ndugu Toms hapa, na ndugu ambao nimekutana nao katika mikutano mbalimbali. Nina furaha sana kuwa nao hapa usiku wa leo pamoja nasi katika kuuombea mkutano. Tulikuwa na wakati mtukufu jana jioni katika kukusanyika kwetu pamoja kidogo.

6 Nami kama ninavyosema tena, ninataka kuomba radhi kwa ndugu zetu wahudumu walio katika mkutano huo mkubwa hapa. Sikukusudia kuingia huku wakati mkiwa na mkutano, lakini nilikuwa tu nikipitia njia hii, naye Ndugu Eddie akasema, “Vema, tunasimama tu siku moja au mbili usiku wakati tukienda zetu.” Nikitumaini kwamba siku moja, kwa ushirikiano mkubwa

miongoni mwa wahudumu wote hapa kisiwani, tunaweza kuwa na mkutano mkubwa mahali fulani.

7 Nilikuja pamoja na Ndugu Eddie kwa marafiki zake Wahindi. Nasi tulikuwa na wakati mzuri sana kule Port Alberni, naamini ndivyo kunavyoitwa, na pamoja na marafiki zetu wa Kihindi, na pia marafiki zetu wazungu. Tulikuwa na wakati mzuri sana kule juu, nasi tunatumaini kurudi hivi karibuni ili kuyaona yote tena.

8 Huu ni mkutano wangu wa kumi na moja mfululizo, nami nimechoka sana. Pia sina budi kuondoka kesho sasa, baada ya ibada, nipate kushuka kufikia . . . sina budi kwenda . . . kushuka hadi Tucson, Arizona, na kutoka huko kwenda, labda, hadi Phoenix. Sina budi kwenda basi kwenye Barabara Kuu ya Alaska nipate kupumzika kidogo. Ninaenda huko pamoja na rafiki, Ndugu Eddie, hapa, na hao wengine. Inanibidi, nirudi kule mnamo Agosti mosi, na kweli niko safarini. Na kisha kurudi na kwenda kwenye nchi za ng'ambo, hadi—hadi Tanganyika, na Uganda, na—na kushuka hadi Afrika Kusini; na, loo, kufanya tu ziara ya kuzunguka ulimwenguni kote, nikijaribu kurudi tena kwenye majira yajayo ya kuchipua, Bwana akipenda, Naye anataka niendelee kujaribu katika uinjilisti ili . . . kwa ajili ya utukufu Wake.

9 Nimeahidiwa, kuanzisha hema zuri, kubwa, jipya, malori, matrela, na kadhalika vyote vikiwa vimelipiwa. Hata haitulazimu, kuchukua matoleo kwa ajili yake. Si ni ajabu hiyo? Kwa hiyo sisi, tukiamini kwamba hayo, kama hayo ni mapenzi Yake ya Kiungu (Sikuzote tunataka mapenzi Yake.), basi nakusudia kufanya yale niliyoahidi sikuzote: kupiga hema katika jamii ambako hakuna miamsho, na kila mtu—na kila mtu akishirikiana; na kufanya mkutano wa asubuhi kwa ajili ya ndugu wahudumu peke yao, kuwazungumzia; mkutano wa alasiri kwa ajili ya mafundisho kwa ajili ya uponyaji wa wagonjwa; kisha ibada ya usiku, ibada ya uinjilisti; na kisha tuachilie kila Jumapili alasiri, na kadhalika, ambapo makanisa mengine yanakuwa na mikutano, tusije tukakatiza mikutano ya kawaida ya hii jamii.

10 Na sikuzote tunataka kufanya hivyo. Na kisha tukae muda kidogo, ninii tu, watu hawaelewi jinsi ya kuponywa, hawaelewi, na ni mara ya kwanza tu kuwa humu, halafu kama tukilifundisha, na kuliingilia katika masomo na kadhalika, nina hakika ingetusaidia sisi sote. Najua ingenisaidia, nami, daima, kupata kuzungumza juu ya Bwana. Na hivyo mimi . . .

11 Ndugu Toms, hapa usiku wa leo, nina hakika ametambulishwa, na kila mtu anamjua kote Saskatchewan, alikuwa mmoja wa wafadhili wangu wa kwanza nilipokuja Saskatchewan yapata miaka kumi na minne, kumi na mitano iliyopita, nadhani. Jamani, ndugu pale, na . . .

12 Ninazungumza kwenye maikrofoni mbaya. Ni nini? Kanisa sahihi, lakini benchi baya, sivyo? Sawa. Na kwa hivyo naona a—ameiweka upande mwingine wa dawati. Kwa kawaida mimi hupaza sauti kidogo, mwajua, na kwa hivyo mimi... Kunizuia nisiwazibe watu masikio humu jengoni, mbona, nadhani aliiweka pale. Vema, tutaachana na hii na kuchukua hii moja kwa moja.

Sasa, ni wangapi wanaompenda kwa moyo wenu wote? Loo, hiyo ni nzuri, nzuri tu.

13 Sasa, kesho alasiri, ili isiingiliane na ibada popote... Sasa, sijui mkutano wa kambi uko wapi, niliusikia tu kabla tu ya kuja hapa, kwamba mkutano wa kambi ulikuwa ukiendelea. Na kwa hiyo, tutakuwa na ibada kesho alasiri yapata saa nane ama tisa. Nadhani wameitangaza.

14 Na—nanyi ambao hamko kwenye mkutano wa kambi, ni kuwachukua tu wale walio wagonjwa na wanaoteseka na ambao hawakuweza kufika kwenye mkutano wa kambi. Hiyo ndiyo sababu tunajiweka wakfu katika kuwaombea wagonjwa. Na sasa, basi kesho alasiri ibada iko hapa. Bwana awe pamoja nanyi na awabariki.

15 Sasa, nataka kusoma Andiko linalopatikana katika kitabu cha Mwanzo na kifungu cha 22 na, mlango wa 22, hasa, na kifungu cha 8:

> *Ibrahimu akasema, Mwanangu, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa:* basi *wakaendelea wote wawili pamoja.*

Na sasa katika kitabu cha Yohana Mtakatifu mlango wa 12 na kifungu cha 32, Yesu akizungumza:

> *Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu.*

16 Na sasa, ili tusichukue muda mrefu katika ibada usiku wa leo, si—sijali, kuwaweka kwa juma zima usiku, kwa sababu katika usiku wa juma, unakosa kazi ya siku moja, sijali hilo, lakini msikose shule ya Jumapili, chochote mfanyacho, nendeni kwenye shule ya Jumapili. Baadhi yenu ni wageni, mbona, wachungaji hawa hapa watafurahi kuwa nanyi katika makanisa yao yaliyo hapa karibu. Watembeleeni asubuhi, watawafaidi mkija kuwasikiliza wakizungumza, na kufahamiana, kwa kuwa tunao U—Umilele wa kuishi pamoja, na kwa hiyo hebu tufahamiane sasa.

17 Na kwa hiyo kumbukeni sasa, sikuzore nimesema, "Ni dhambi kuwatuma watoto wako kwenye shule ya Jumapili." Kila mtu anajua hilo. Kamwe usiwahi, chochote ufanyacho, usiwatume watoto wako kwenye shule ya Jumapili. Ni kosa, wapeleke. Hiyo ni kweli. Daima wapeleke. Usiwatume tu, nenda uwe mfano pia. Wapeleke kwenye shule ya Jumapili, nenda

pamoja nao. Lakini, usiwatume tu, hilo ni kosa, kuwapeleka ni sawa, maana uko huko pamoja nao.

18 Na sasa, kesho alasiri tutajaribu, Mungu akipenda, kuwaombea wagonjwa na wanaoteseka, wengi kadiri tuwezavyo, au kikundi, isipokuwa kiwe kikubwa mno, maadamu ni kundi dogo tu namna hii, mbona, tunaweza kufanya hivyo kwa urahisi. Kwa hiyo, kama una watu wako wagonjwa, na unataka kuwaleta kwa ajili ya maombi kesho alasiri, tutafurahi kuwaombea.

Sasa, ninawatakeni, muwaalike ndugu ambao ni wachungaji wenu, pia, waje wakatutembelee kesho baada ya shule ya Jumapili, kama akiweza.

19 Sasa, ninataka kutoa katika somo hili la Maandiko kutoka katika Mwanzo mlango wa 22, kifungu cha 8: "Mungu atajipatia Mwenyewe dhabihu." Na kisha katika Yohana Mtakatifu 12:32, ambapo nina muhtasari wangu na kadhalika, na Maandiko yangu yameandikwa ambayo nilitaka kuzungumzia: "Mimi, nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote Kwangu." Ninataka kuchukua somo kutoka kwa hilo, *Mungu Anayo Njia Iliyoandaliwa.*

20 Sasa, mnajua, nina furaha sana kujua ya kwamba kuna njia iliyoandaliwa. Mnaona, kuna—kuna njia mbili tu za kitu chochote: hiyo ni njia nzuri na njia mbaya; na hiyo ni njia yako na njia ya Mungu. Huwezi kuwa na njia yako mwenyewe na kuwa katika njia ya Mungu; wala huwezi kuwa katika njia ya Mungu na kufanya upendavyo. Unaona? Kwa hiyo, ni moja au nyingine: ama ni njia yako au njia ya Mungu; ni mawazo yako au Neno la Mungu. Unaona? Lazima ukubali moja. Huwezi kuchukua mawazo yako mwenyewe. Kwa hiyo, mwanadamu alizaliwa akiwa mwenye kushindwa, na daima amekuwa mtu aliyeshindwa. Kwa hivyo, kwa nini kujaribu kutegemea ufahamu wako mwenyewe? Kwa nini usichukue njia ya Mungu kwa ajili yake? maana Yeye daima hukutoa ukiwa sawa.

21 Na sasa, Yeye anapoandaa njia na watu hawatembei katika njia hiyo, basi si kosa la Mungu. Kwa mfano, hili jiji hapa, wana mawasiliano ya taa, taa za kusimamisha, nalo jiji limeziweka hizo kwenye makutano hatari. Vema, kama taa hiyo nyekundu ikiwaka na kusema, "Usiende sasa," nawe uipitie hiyo taa nyekundu, unaona, hujaja kwa njia iliyoandaliwa, nawe ukipata ajali, usilaumu jiji, waliweka onyo pale, usimlaumu mtu aliyekugonga, ulilisababisha mwenyewe. Unaona? Na unaona, hiyo ni wewe ukitumia njia yako, au njia iliyoandaliwa.

22 Kwa mfano, tutakapoanza kwenda nyumbani kesho, vema sasa, vipi kama nikisema, "Hebu nione ninakoishi sasa, ninaishi kitu kama mashariki, na kusini, na kadhalika, nitaelekea huko moja kwa moja, nichukue njia ya mkato, kwa sababu sina budi kuharakisha kwenda nyumbani, vema, je, nitaenda moja kwa

moja hivyo"? Loo, ningejipata hapa kwenye Mlangobahari wa Puget mahali fulani, nimezama baharini, au ningejipata kwenye uwanja uliojaa matope. Siwezi kufanya hivyo. Nikifanya, mimi, si—sitafika popote kamwe.

23 Kweli, vile tu ninavyopaswa kufanya, ni kuchukua ramani ya barabara, na kuna . . . barabara kuu zimeandaliwa nipate kusafiria; ikiwa nitachukua tu hiyo ramani ya barabara, na kufuata ramani ya barabara, nita—nitafika huko. Mnaona? Nikifuata tu hizo alama, sina budi kufika huko. Inaweza kuonekana mbaya kwa mawazo yangu, lakini barabara tayari imeandaliwa. Na sasa, mawazo yangu, ikiwa ni kinyume na jinsi barabara ilivyoandaliwa, basi hebu nisiyawaze mawazo yangu, hebu niende jinsi ishara zinavyoelekeza, nami nitafika huko.

24 Ndivyo ilivyo kwa njia yetu ya kwenda Mbinguni, tuna mawazo yetu wenyewe, lakini tukiyatumia hayo, tutajikuta tumekosea kabisa, tumepatikana na ajali mahali fulani, lakini kama tutachukua njia ambayo Mungu ametutengea, tutafika kule hakika kama chochote kile, maana Mungu anayo njia.

25 Sasa, hebu turudi kwenye baadhi ya njia za Mungu kwa njia rahisi ambayo watu wangejua. Je, umewahi kumwona maskini kuku akijaribu kuja humu duniani? Anafanya nini? Ndani ya ganda hilo anasimama pale na kudonoa ganda hilo mpaka anajiweka huru. Ni nini? Njia iliyoandaliwa na Mungu. Alikuwa na mdomo, kabla hajaweza kugonga kwenye hilo ganda, alikuwa na mdomo, maana Mungu alimpa mdomo, apate kufanya kazi katika njia ya Mungu iliyoandaliwa. Mnaona?

26 Loo, Yeye ni Baba mpendwa, mnaona, Yeye hufanya kila kitu sawa kabisa. Kwanza, ilimbidi kuotesha mdomo juu ya ndege, huyo kuku, anayezaliwa ndani ya yai; Yeye hana budi kumtengenezea njia ya kuifuata njia iliyoandaliwa ya kutoka nje. Mnaona jinsi Mungu afanyavyo? Yeye hufanya njia iliyoandaliwa, na jambo pekee tunalopaswa kufanya, ni kufuata maagizo Yake, nasi tunatokea sawa kabisa, daima, kila wakati. Naam, bwana. Yeye hudonoa akatoka, kwa sababu anakuja kwa njia ya Mungu iliyoandaliwa.

27 Mara nyingi nimeshangaa, ninapokuja hapa katika majira ya kupukutika mwakani katika ziara ya kuwinda, na ninastaajabia, ninapopanda juu ya milima mirefu hapa na kuwatazama bata, yapata tu wakati wa kuhama, na bata bukini. Sasa, wanatoka kusini, wanakuja hapa na kuingia kwenye vinamasi hivi vichafu, vilivyojaa matope, na kujitengenezea kiota, wanataga mayai yao, na kuangua watoto wao. Vema, maskini vifaranga hivyo vya bata, walilelewa kwenye dimbwi hilo, ama ziwa, wala hawajui kitu kingine ila ziwa hilo, alizaliwa humo majira ya kuchipua yaliyopita, ameishi humo majira yote ya kiangazi, amepata riziki yake, na *kwa njia moja au nyingine*, wakati ninii, mnamo mwisho wa Agosti au Septemba, wakati theluji inapoanguka

milimani, na huo upepo wa baridi unashuka ukivuma chini katika nchi hiyo ya mbuga pana, aliko maskini bata huyo, anajua kuna jambo linakaribia kutukia.

28 Sasa, anafanya nini? Wote wanaanza kukusanyika, na huko nje katikati ya dimbwi hilo atatokea maskini bata dume aliyezaliwa msimu huo wa kuchipua humo dimbwini, ataenda moja kwa moja katikati ya dimbwi hilo, ainue maskini mdomo wake hewani, na kufanya, "Hong', hong'. Hong', hong'," na kila bata kwenye hilo dimbwi atamjia. Mnaona?

29 Sasa, Mungu ameweka silika, silika katika huyo bata kumwambia kwamba kitu hicho kitaganda, naye atafia humo. Kwa hiyo, hawezi kukaa hapa, wala hajawahi kuwa popote ila hapa, bali Mungu ana mahali pengine pa yeye kwenda. Hivyo yeye. . . Ikiwa ana mahali pengine palipoandaliwa huko Louisiana na Texas kwenye mashamba ya mpunga, baada ya kula shayiri zote kutoka kwako alivyoweza, basi anashuka sasa kwenda kwenye mashamba ya mpunga ku—kuishi huko Texas, na—na huko chini. Vema, sasa, amezaliwa humu katika ziwa hili, hajui lolote juu yake, bali ana silika aliyopewa na Mungu, njia ya Mungu iliyoandaliwa inayomwambia kwamba shida iko karibu, ndipo anaanza kuihisi hewa.

30 Na si tu kwamba. . . Iwapo itabidi wahame, mmoja angeenda huku na mmoja angeenda kule, Mungu aliwapa kiongozi. Ni aibu kwamba mwanadamu, pamoja na Roho Mtakatifu, hana akili nyingi kama vile bata alivyo na silika. Kamwe siwezi kusema. . . Bila shaka, bata anaamini katika ninii wake wa Mungu. . . utoaji, lakini mwanadamu haamini. Mnaona? Tunajaribu kuchukua mafanikio ya kujibunia ili kujiepusha na shida, wakati Mungu alitupatia Roho Mtakatifu tupate kujiepusha na shida. Mnaona? Hiyo ni kweli. Na sasa, tunapohisi shida hewani, kuna jambo moja tu la kufanya, hilo ni kumsikiliza Kiongozi. Naye Roho Mtakatifu ndiye Kiongozi, Yeye alitumwa kuliongoza Kanisa.

31 Na sasa, kumbukeni, maskini bata huyu hajawahi kutoka kwenye dimbwi hilo, lakini kila bata kwenye hilo dimbwi anajua kwamba yeye ndiye kiongozi. Basi wakati maskini jamaa huyo, asubuhi moja hiyo silika inampanda sana hivi kwamba anatoa mlio mwingine, anaondoka humo dimbwini, anasema, "kwaheri," na kila bata anamfuata. Yuko juu hewani, hajui njia ya kwenda huko juu, lakini namna fulani ya njia iliyoandaliwa na Mungu, anauelekeza maskini uso Louisiana, naye huyo anaenda zake, naye anafika huko. Kwa nini? Anaitumainia njia ya Mungu iliyoandaliwa kwa ajili yake, hiyo ndiyo sababu anaweza kufaulu, ameiamini njia ya Mungu iliyoandaliwa. Angalieni, jinsi linavyopendeza.

32 Waangalie hao mabata bukini, jinsi wanavyopanda kutoka pale na kusongamana. Ninapenda tu kuwasikia katika majira

ya kupukutika mwakani. Wanapitia Indiana wakitoa mlio wawezavyo kwenda, maskini kiongozi mmoja pale akiwa mbele, huku pua imechomoza moja kwa moja kuelekea Louisiana, naye huyo anaenda zake, hajawahi kuwa huko hapo kabla, hajui kuna nini huko chini.

33 Kama wana wa Israeli walivyoongozwa na ile Nguzo ya Moto, waliinuka kutoka Misri, hawakuwa wamewahi kwenda huko nje hapo kabla, bali walikwenda moja kwa moja mpaka kwenye nchi ya ahadi, kwa sababu walikuwa wakifuata Nguzo ya Moto, yule Kiongozi aliyewekwa na Mungu. Walikaa moja kwa moja katika njia ya Mungu iliyoandaliwa.

34 Loo, ni vibaya sana kwamba sisi wanadamu tunaikosa sana, kwa sababu hatujui Kiongozi wetu ni Nani. Hilo ndilo jambo pekee, tunajaribu kuchukua wazo letu wenyewe, daima tunakwama mahali fulani na kupata ajali.

35 Sasa, bata na bata bukini huenda kusini, nao wana kiongozi aliyeandaliwa. Mungu, ikiwa atakutuma popote penye njia fulani, ni juu ya Mungu kukupa Kiongozi wa kuongoza njiani. Sikuzote. Naam, bwana. Mungu hukupa. Kama utaangalia tu maumbile, hayo yalikuwa ndiyo Biblia yangu ya kwanza, kuangalia maumbile, kama utaangalia, kamwe hutamkosa Mungu kama unaweza kuangalia maumbile.

36 Nimekuwa na majaliwa ya kusafiri ulimwenguni kote, na katika mahekalu ya Budha, na—na Muhammad, na Majaini, na Makalasinga, na kadhalika, lakini kila mmoja wao ana falsafa, lakini zinatokana na wasiwasi, na loo, sijui nyote mnaweza kuuita nini, kuzaliwa tena katika kiumbe kingine, na kila namna ya mambo, lakini Ukristo umejengwa juu ya kuzikwa na kufufuka, hiyo ndiyo kanuni.

37 Sasa, ufufuo si kumweka mwingine badala yake, ufufuo ni kumwinua yule yule aliyeshuka. Sasa, kama kipande hiki cha karatasi kikianguka, na kufika sakafuni, sasa, kama nikikichukua tu kipande hiki cha karatasi na kukiweka mahali pa kile, huo sio ufufuo, huko ni kubadilisha, bali ufufuo ni, kilete kiki hiki kilichoanguka, huo ndio ufufuo.

38 Sasa, kitu chochote kinapotumikia kusudi la Mungu, hakina budi kukaa katika njia ya Mungu iliyoandaliwa. Hebu tuchukue maua haya, yaliwekwa hapa kutumikia kusudi la Mungu. Sasa, ukiyakata *hivyo*, unafikiri ndio mwisho wake, sivyo. Mungu huyajali maua Yake. Ikiwa utaangalia, ua zuri, jinsi . . . Nimeona ninyi Wakanada hapa, jinsi mlivyo na mabustani haya mazuri na maeneo mazuri sana ya maua.

39 Sasa, baada ya kitambo kidogo, yatakuwa maua machanga, maua ya siku nyingi, maua ya makamo, lakini kutakuja jalidi kote nchini usiku mmoja, mauti. Nayo italipiga ua hilo, haijalishi lina umri gani; mauti hayana upendeleo wa umri, mtu, au uwezo, mauti huwapata wote. Nini kinatokea? Maskini jamaa

huyo anatoa uhai wake. Nini kinatokea basi? Petali zinaanza kupukutika kutoka kwake kesho yake asubuhi, linakwisha. Kutoka humo hudondoka mbegu ndogo, inaanguka ardhini, ndipo unakuja msafara wa mazishi. Huenda usiamini, lakini Mungu ana msafara wa mazishi kwa ajili ya maua Yake. Je, ulijua hilo? Sasa angalieni, baada ya jalidi kupiga, ndipo mvua ya masika inakuja, Mungu anatuma mawingu kote, na kulia matone makubwa ya maji yakaanguka chini, na kuizika maskini mbegu hiyo.

40 Mnaona, tunajaribu kulifanya jambo gumu sana. Hiyo ndiyo shida siku hizi, jinsi ambavyo kanisa sikuzote limetoka kwenye njia iliyoandaliwa, wamejaribu, wakamfanya Yeye kuwa mgumu sana, kana kwamba hawana budi kuelimishwa ili kuingia ndani yake; huelimishwi ukaingia ndani ya Kristo, unazaliwa ndani ya Kristo kwa Roho . . .?. . .

41 Sasa, Mungu huwatuma wenye kulia na waombolezaji, ambao ni maji, nayo yanatiririka chini kama machozi makubwa na kuizika maskini mbegu hiyo. Hiyo inaingia chini ya ardhi, yanapoisukuma chini, ndipo upepo wa theluji ya kipupwe unakuja, unaenea nchi nzima. Ile petali ndogo imetoweka, majani yanaanguka, ubua umekwisha, balbu imekauka, kisha maskini hiyo mbegu inaganda na kupasuka, nyama inatoka ndani yake; maskini ua dogo, inaonekana kama ni mwisho wake. Loo, la, sio mwisho wake, wakati jua hilo lenye joto linapoanza kurudi tena, dunia ikijiandaa kupata jua, kuna chembe ya uhai mahali fulani katika uchafu huo ambayo hakuna sayansi imewahi kuipata, ua hilo linaishi tena. Kwa nini? Lilitumikia kusudi la Mungu katika njia ya Mungu iliyoandaliwa, Naye akafanya njia lipate kuishi tena.

42 Na kama alifanya njia kwa ajili ya ua kuishi tena ambalo lilitimiza kusudi Lake, ni zaidi sana vipi Yeye amefanya njia kwa ajili ya mwanamume au mwanamke kuishi tena ambaye hutumikia kusudi Lake, anayetembea katika njia Yake iliyoandaliwa. Rahisi sana, ili tu kutazama.

43 Angalieni miti, jinsi majani yanavyojitokeza pale na kuning'inia. Hivi majuzi tu, miezi michache iliyopita, nilimpoteza mama yangu na, mama yangu mtauwa, mkongwe, naye alikuwa amelala kitandani, akiondoka, nami ni—nilikuwa mbali huko Canada, huku katika—katika British Columbia, nami nilikuwa nimerudi. Mama alikuwa mgonjwa nami nikaenda kumwona, walikuwa wamempeleka hospitalini, akasema, "Billy, huu ndio mwisho, Mwanangu."

Nikasema, "Loo, mama, jamani, huo sio mwisho."

Akasema, "Naam, ndio."

44 Nisingeweza kukata tamaa, niliendelea kuomba, naye akazidi kudhoofika wakati wote, Mungu hakuniambia chochote, nikasimama pale. Mara nyingi nimetoa hili tamshi mimbarani,

ninyi watu mnaojua, mara nyingi nimesema, “Kama mama yangu mwenyewe alikuwa amelala hapa akifa, ningewezaje kumwambia jambo moja isipokuwa Mungu aliniambia kwanza? Ninaweza tu kusema kama Mungu anavyosema niliseme.” Hapo jambo hilo likatimia, mimi nikimwombea mama yangu.

45 Dada yangu ndiyo kwanza ampokee Roho Mtakatifu, naye, ndiye msichana pekee, loo, lilimtia wasiwasi. Nilikuwa huko nje siku moja na, kumwona, naye Dada alikuwa pale, ndipo Mama akatuangalia, akasema, “Wangu wa kwanza na wa mwisho.” Hiyo ilikuwa, nilikuwa kifungua mimba, Delores alikuwa kitinda mimba; kulikuwa na wavulana tisa na msichana mmoja, naye huyo msichana alikuwa wa mwisho.

46 Na kwa hiyo, Mama akasema, “Billy,” kasema, “wewe ndiye uliyehakikisha kwamba sikukosa chakula, ulininunulia nguo zangu na kunilisha baada ya Baba kuondoka.” Kisha kasema, “Delores, umekuwa mtamu kwangu, umekuja kwangu, na kunisaidia kufua, na kuisafisha nyumba yangu, na kadhalika wakati sikujisikia vizuri.”

Ndipo mimi na Delores tukaangaliana, na kusema, “Loo, Mama, hilo ni sawa.”

Kisha nikasema, “Baadhi yao wameuvunja moyo wako, Mama, baadhi ya hao wavulana walikunywa pombe, na hilo likauvunja moyo wako.”

47 Akasema, “Billy, yote huenda kufanya maisha ya mwanadamu.” Mama huyo asingeweza kusahau, haidhuru walifanya nini, ni mamoja. Kwa hiyo, akasema, “Na, Billy, jambo moja tena,” kasema, “wewe ndiye uliyeniongoza kwa Kristo, Yule anayemaanisha yote katika yote kwangu sasa.”

48 Nami nikasema, “Mama, nilienda kanisani, nalo kanisa likasema kwamba Mungu alikuwa katika kanisa Lake, kasisi alisema.” Nami nikasema, “Kisha ni—nikaelewa ya kwamba Mungu alikuwa katika Neno Lake, nami nimedumu na Neno, nimejaribu kuwafundisha Neno.”

Naye akasema, “Sasa, ndio wakati malipo yanapatikana.”

Delores akaenda nyumbani, akanipigia simu, akasema, “Bill, siwezi kuvumilia kuona Mama akituacha.”

Nikasema, “Delores, ni nini kinachokufanya useme jambo kama hilo?”

49 Akasema, “Siwezi kustahimili kumwona Mama akienda, ndiye mama pekee tuliye naye, na ndiye pekee tutakayewahi kuwa naye.” Tena kasema, “Wewe huyu hapa na umri wa miaka hamsini na mitatu nami ishirini na saba.” Kasema, “Tu—tutalistahimilije, Bill? Tumekuwa naye maisha haya yote.”

50 Nikasema, “Delores, angalia dirishani ambapo umeketi kwenye simu yako, mkono wako wa kushoto. Unaona nini? Je, kuna mti umesimama hapo, mti mkubwa mno wa mwaloni?”

Akasema, “Ndiyo.”

Nikasema, “Miezi miwili iliyopita majani yote yalikuwa mazuri na ya kijani.”

“Ndiyo.”

Nikasema, “Sasa yana rangi gani, Delores?”

Naye akasema, “Ni ya kahawia, na ni mekundu, manjano, na kijani.”

Nikasema, “Kwani kuna nini?”

Akasema, “Uhai unaondoka kwenye hilo jani.”

Nikasema, “Kweli.” Nikasema, “Ni lini ulikuwa wa kupendeza zaidi?”

Akasema, “Sasa hivi.”

51 Nikasema, “Katika mauti yake.” Amina. “Ina thamani machoni pa Bwana mauti ya watakatifu Wake,” kuwaona hao watakatifu wa kale wakifikia mwisho, hadi dakika ya mwisho.

52 Wakati Mama asingeweza kuongea tena, nilisema, “Mama, ni sawa kama unaweza. . . nataka,” nikasema, “kama mvulana wako mhubiri, nataka kukuuliza, Kristo anamaanisha nini kwako?”

Naye angesema, “Yote katika yote, yote katika yote, Yeye ni mpendwa zaidi sasa kuliko hapo awali.”

53 Na wakati asingeweza kuzungumza tena, ningesema, “Mama, huwezi kuongea tena, unaondoka sasa katika dakika chache tu. Ninataka kuikabidhi nafsi yako kwa Mungu, nikisimama hapa, Mama, kama huwezi kuzungumza nami sasa, kama Kristo angali anamaanisha kila kitu kwako, unapokaribia sasa kufa, kama huwezi kuongea, pepesa macho yako.” Naye angepepesa macho yake juu chini, kisha akaenda kukutana na Mungu.

54 Loo, jamani, jamani! “Wa thamani machoni pa Bwana,” ushuhuda huo mzuri, huku Shetani amesimama pale, aseme, “Nitawafanya Bill na Delores, hao, wakupe kisogo, niruhusu nimchukue na kumtesa kidogo.” Lakini, loo, jamani, kumwona mtakatifu huyo mkongwe akishikilia moja kwa moja hadi mwisho huo na kwenda kukutana na Mungu, kama tu jani linavyoondoka.

55 Ninamtazama rafiki yangu mpendwa aliyeketi hapa, ambaye zamani alikuwa Shahidi wa Yehova, naye ni. . . jina lake ni Banks Wood, naye ni jirani yangu. Naye alikuja, sio. . . Siku moja, alipokuja kwa mara ya kwanza, yeye na mke wake, walikuwa na mvulana aliyekuwa na polio, naye alikuwa kwenye mkutano wa Texas, kwanza kule Louisville, ambako alimwona msichana, aliyekuwa akigeuka kuwa chaki, au, ilikuwa ni jiwe, aliponywa, akipanda na kushuka vipandio mbio, ikawashangaza madaktari wote na kila kitu. Walikuwa wamemleta mvulana

wao mwenye polio huko Texas, huko ndiko alikopigwa picha Malaika wa Bwana, ile Nguzo ya Moto. Halafu basi, baada ya hapo nikaenda Norwe na Uswidi, nikarudi, nilikuwa huko Ohio, wakamleta huyo mvulana kule, huku siwajui.

56 Usiku mmoja Roho Mtakatifu akanena na kusema, “Huyo mvulana mdogo mwenye shati la manjano hapo nyuma ameponywa, BWANA ASEMA HIVI.” Na wakati huo Roho Mtakatifu akashuka, akaunyoosha mguu huo uliopinda, mkamilifu kabisa katika. . .Je, David yuko hu—humu jengoni usiku wa leo? La, alienda nyumbani, sivyo? Huyu ni baba yake, inua mkono wako, Banks. Mama yake ameketi hapa mahali fulani. Uko wapi, Dada Wood? Kama. . .Hao hapo kama mashahidi.

57 Vema, wananipenda sana hata wakahamia huko, jirani yangu kwangu, nao ni jirani kabisa wa Matendo 2:4 pia, ndivyo walivyo kweli, wote wawili wakimpokea Roho Mtakatifu. Na familia yake yote, karibu kila mmoja wao wakiwa wasomaji katika Mashahidi wa Yehova, kupitia kwa maono na nguvu za Mungu, akamwelekeza kila mmoja kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu. Watu wa mkewe wote wakiwa ni Methodisti, wanawake wazuri, wanaume wema, na kila kitu, na kila mmoja wa watu wake, kundi zima, limeingia na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, isipokuwa mmoja. Kumwangalia Mungu. . .

58 Nami na Ndugu Banks tunapenda kuwinda kuchakulo. Sijui kama mtu yeyote. . .Ni wangapi waliowahi kwenda kuwinda kuchakulo? Loo, jamani! Kwani mnatoka sehemu gani ya Kentucky kwa vyovyote vile? Mnaona? Wala, hakuna uwindaji kama huo, hakuna mahali popote. Nasi, tunawinda kuchakulo kwa bunduki ya .22, kulenga shabaha kwenye yadi hamsini, kuyalenga macho, wala hatupati kuchakulo wengi sana kupita kiasi, lakini tunakuwa na wakati mzuri sana ninapoenda likizoni.

59 Basi, siku moja kule chini, ilikuwa, majira hayo ya kupukutika yalikuwa makavu sana, miaka miwili iliyopita, nasi tulikuwa tukipiga kambi huko nje, tulikuwa hatujaoga kwa majuma kadhaa, na ndevu zimetapakaa usoni mwetu, na damu ya kuchakulo, tulikuwa tumechafuka kweli. Lakini, nilikuwa nikipumzika kutoka kwenye mikutano, kwa namna fulani nikiondoka kuingia kwenye maumbile, sikuzote ninamwona Mungu katika maumbile Yake, nikiangalia njia Yake aliyoiweka. Angalieni. Ndipo basi, kulikuwa kukavu sana, tunapoingia msituni, hiyo miti iliyotandaa, jani moja likivunjika, nawe wanena kuhusu Houdini kuwa bingwa wa kutoroka, yeye ni mwanagenzi ukimlinganisha na mmoja wa hao kuchakulo, [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] ametoweka, namna *hiyo*, na kulenga risasi ya bunduki, na halafu jicho, ni jambo gumu kufanya.

60 Kwa hiyo, Ndugu Banks akasema, "Unajua, najua mahali ambapo kuna mtu ambaye ana ekari mia tano za misitu zote zikiwa vibondeni." Ni wangapi wanaojua kibonde ni nini? Vema. Na, huko ni chini kwenye kitu kama bonde, ambamo maji hupitia, akasema, "Tungeweza kushuka kule na kutembea." Kwa hiyo, tukashuka kwenda kumwona mtu huyu, akasema, "Jambo pekee ni kwamba, mtu huyu ni kafiri, mtu mbaya sana asiyeamini."

61 Vema, tulipitia makondeni na kila kitu mpaka tukarudi mahali pake. Basi tuliporudi mahali ambapo huyu kafiri, asiyeamini, aliishi, huyo hapo ameketi chini ya mti, yeye na mzee mwingine waliketi pale nje, wamezishusha kofia zao, wakitafuna tumbaku na kutema mate, namna hiyo. Kwa hiyo, Ndugu Wood akashuka kutoka kwenye gari, akaenda, na kusema, "Je, ninaweza kuwinda kuchakulo kwenye eneo lako kwa muda kidogo?"

Akasema, "Jina lako ni nani?"

Akasema, "Wood."

Akasema, "Wewe ni Wood yupi?"

Naye akasema, "Banks."

Akasema, "Wewe ni mvulana wa Jim Wood?"

Akasema, "Naam." Huyo alikuwa ni baba yake.

Akasema, "Vema, mvulana yeyote au mtu yeyote wa Jim Wood anakaribishwa mahali popote katika eneo langu wanapotaka kuja."

Kwa hiyo, akasema, "Nilikuja na mchungaji wangu. Je, anaweza kuwinda pia?"

Maskini mzee huyu akatema mate na kusema, "Wood, humaanishi kuniambia uliharibika sana, hata inakubidi kubebana na mhubiri popote uendapo?"

Na kwa hivyo, nikawazia wakati wangu wa kutoka nje ya gari ulikuwa umewadia, hivyo nikatoka kwenye gari na kuzunguka pale, nikasema, "Mu hali gani?"

Akasema, "Nawe ni muhubiri ati?"

Nikasema, "Naam, bwana."

62 Na kabla Ndugu Wood hajapata nafasi ya kunitambulisha, mbona, akasema, "Unajua, shida na nyinyi jamaa," akasema, "mnabwekea mti usio." Mnajua ni nini, mbwa kuuni anayebwekea mti usio, yeye ni mwongo, mnaona, naye kuuni ameondoka, wala habwekei chochote. Kwa hiyo, akasema, "Nyie jamaa mnabwekea mti usio."

Nikasema, "Unamaanisha nini?"

63 Hakuamini kulikuwa na kitu kama Mungu, wala hakujua lolote kukihusu. "Vema," nikawazia, "sasa, mzee huyo si mbaya, hakusudii kuwa hivyo."

64 Akasema, "Wanazungumza juu ya *hili*, na wanazungumza juu ya *lile*, na hakuna kitu kwake. Nimekuwa papa hapa, wala sijawahi kuona kitu kama hicho, ninaweza kuangalia juu *kule*, wala sioni chochote, naangalia *huku*, sioni chochote." Kasema, "Kwa nini, wao. . . "

65 Mnaona, shida yake ni kwamba, ni kama tu watu wanaokuja kwenye mkutano mmoja, kuna miti mingi sana hata huwezi kuona misitu. Ni hayo tu. Unaona? Kwa hiyo basi, aliketi pale, mwajua, kitambo kidogo, nami nikawazia, "Bwana, kama utanisaidia tu sasa, labda tunaweza kumshika jamaa huyo mzee kwa ajili ya Ufalme wa Mungu."

66 Basi kulikuwa na mtofaa umesimama pale, nao manyigu (Ni wangapi wanaojua manyigu ni nini?), alikuwa. . . walikuwa wakila hayo matofaa, nami nikanyoosha mkono na kuokota, nikasema, "Je, ninaweza kuchukua moja ya matofaa haya?"

67 Kasema, "Karibu, manyigu wanayala." Kwa hiyo, nikaanza kulisugua, namna *hiyo*. Naye akasema, "Kulikuwa na mhubiri mmoja, wakati mmoja, hapa yapata miaka mitatu iliyopita, ama minne, aliyekuja hapa kwenye mji mdogo unaoitwa Acton." Kisha kasema, "Acton ni mahali padogo sana ambapo wana kambi ya Wamethodisti." Kasema, "Mhubiri huyu alishuka kutoka Indiana, naye alipajaza mahali hapo na msongamano wa watu, hapo siku tatu usiku."

68 Naye akasema, "Maskini bikizee *Jina fulani* huku juu kilimani alikuwa na kansa tumboni mwake, na," kasema, "alikuwa mahututi sana wasingeweza kumweka tena kwenye maliwato ya kitandani, iliwabidi kutumia shuka la kuvutwa." Kisha kasema, "Mimi na mke wangu tungeenda huko mara mbili kwa siku na kumtengenezea kitanda chake." Kasema, "Madaktari walimkatia tamaa afe majuma kadhaa kabla ya hapo na," kasema, "hakuna kitu kingeweza kufanywa, ilikuwa vigumu kwake kuongea tena, asingeweza hata kuweka maji yenye joto tumboni mwake."

69 Kisha kasema, "Dada yake alishuka kwenda kwenye mkutano huo usiku huo na," kasema, "mhubiri huyu, akisimama pale, kamwe hakuwahi kuwa katika nchi hii hapo awali maishani mwake, akatazama nyuma juu ya kusanyiko na kusema, 'Mwanamke huyu anayeketi nyuma hapa anaitwa *Fulani-wa-fulani*. Alipotoka nyumbani usiku wa leo, aliweka kuto-. . . alichukua kutoka kwa droo ya kabati la nguo upande wa kulia leso ndogo yenye mchoro wa bluu ndani yake, akaiweka kwenye kibeti chake. Endapo ana dada mgonjwa. . . *Ana* dada mgonjwa anayeitwa *Fulani* anayeishi hapa juu, naye yuafa kwa

kansa. BWANA ASEMA HIVI, chukua leso hii uende ukaiweke juu ya dada yako naye atapona.'"

70 Kisha kasema, "Huyo mwanamke akainuka kwenye kiti pale alipokuwa ameketi, akaenda na kuweka leso hiyo juu ya mwanamke huyo." Naye akasema, "Mbona, wao...Nilifikiri walikuwa na Jeshi la Wokovu kule juu ya kilima." Kasema, "Sikuwahi kusikia mayowe mengi hivyo, yapata saa sita usiku huo."

71 Vema, lilikuwa ni kundi lao kule juu wakiweka leso juu ya maskini huyo bi-kizee, naye akapona, kulingana tu na Neno la Bwana, aliinuka, akirukaruka kote, akipaza sauti, akimsifu Bwana.

72 Kisha kasema, "Kesho yake asubuhi, mimi na mke wangu tukaenda huko." Kasema, "Ilikuwa imechelewa, yapata usiku wa manane, tuliwazia huyo bi-kizee, tulikuwa tukimtazamia afe dakika yoyote kwa vyovyote vile, tulifikiri hao walikuwa watoto wake wakilia, kwamba tayari alikuwa ameaga dunia." Kisha kasema, "Tulikwenda huko kesho yake asubuhi, huyo hapo yeye na mume wake wameketi, mezani wakila sambusa za matofaa yaliyokaangwa na kunywa kahawa." Tena kasema, "Anafanya kazi zake mwenyewe na za jirani."

Nikawazia, "Loo, loo. Hiyo ndiyo sababu...Nina furaha ulisema hivyo."

Ndipo Ndugu Banks akaanza kusema, "Naam, huyo..."

Mimi, "Uh-uh. Usininii. Mnaona? Usininii." Nikasema, "Kumbe?"

Akasema, "Naam, ndivyo ilivyo."

Nikasema, "Kweli huamini hilo."

73 Akasema, "Panda moja kwa moja kule juu upate kujua." Mnaona, alikuwa akinihubiria tena wakati huo. Mnaona? Mnaona? "Nenda moja kwa moja kule juu upate kujua, jina lake ni *Fulani-wa-fulani*, anaishi karibu sana na ile kona."

Yule mzee mwingine aliyeketi pale, akasema, "Hiyo ni kweli." Mnaona?

Nami nikasema, "Unamaanisha hiyo ni kweli?"

Kasema, "Vema, nenda ukajionee."

Nikasema, "Jamani!" Nikasema, "Jina la jamaa huyo lilikuwa ni nani?"

Kasema, "Sijui." Kasema, "Nalisahau." Kasema, "Mhubiri fulani kutoka huko Indiana," akasema.

Nami nikasema, "Naam, bwana." Na, nilikuwa nikila tofaa hilo, mwajua, nami nikasema, "Hilo ni tofaa zuri."

Kasema, "Loo naam." Kasema, "Ni tamu sana, tunatia koponi kutoka kwake kila mwaka."

Nikasema, "Mti huo una umri gani?"

"Loo," akasema, "sisi. . .niliupanda mti huo hapo mimi mwenyewe yapata miaka hamsini iliyopita, kitu kama hicho." Alikuwa na sabini na sita, nafikiri ndivyo.

Nikasema, "Naam, uh-huh." Nikasema, "Nataka kukuuliza swali."

74 Naye akasema, "Naam, bwana." Ndiyo kwanza amalize kusema, "Kama mhubiri huyo akirudi hapa kamwe, ilionekana kana kwamba alikuwa anajua anachozungumzia." Akasema, "Nitamwuliza: Alijuaje kuwa mwanamke huyo alikuwa katika hali hiyo, naye alijuaje kuwa atapona?"

Nami nikasema, "Unasema uliupanda huo mti hapo zamani sana?"

"Naam."

75 Nikasema, "Nataka kukuuliza swali. Ni karibu tu katikati ya Agosti, hatujapata hata usiku wenye baridi. Kwa nini majani hayo yanapukutika kutoka mtini?"

"Loo," akasema, "Uhai umeyaacha."

"Loo," nikasema, "kumbe? Vema, uhai ulipatwa na nini?"

"Loo," anasema, "ulishuka ukaingia kwenye mizizi ya huo mti."

Nikasema, "Kwa nini ushuke huko?"

Akasema, "Vema, usiposhuka, utakufa, majira ya baridi kali yatauua, chembe ya uhai haiwezi kukaa juu ya mti huu hapa."

Nikasema, "Loo. Vema," nikasema, "ni nini kinachosababisha ushuke kabla ya baridi yoyote?"

"Vema," akasema, "unashuka tu."

Nami nikasema, "Naam, sasa . . . "

Akasema, "Ni maumbile tu, unashuka tu."

76 Nikasema, "Vema, kama nikichota ndoo ya maji na kuiweka hapa kwenye hicho kisiki cha nzige, je, majira ya kupukutika yatakapokuja, maji hayo yatatoka kwenye hiyo ndoo yashuke chini kabisa ya hicho kisiki, kisha majira yajayo ya kuchipuka, yalete ndoo nyingine ya maji?"

Kasema, "La."

77 Nikasema, "Basi hapana shaka kuna Akili fulani, mti huo hauna akili, ni—ni mti, mmea, hapana shaka kuna namna fulani ya Akili ya kuufanya ushuke kuuficha uhai wake, kisha urudi kukuletea lundo jingine la matofaa."

Akasema, "Vema, unajua nini?" Akasema, "Kamwe sikuwa nimeliwazia namna hiyo."

78 Nami nikasema, "Nakwambia, wewe tafakari hayo, na wakati wowote unapoweza kupata Akili inayouambia mti huo,

'Pukutisha jani lako, harakisha urudi chini mizizini, na ukae humo, na majira yajayo ya kuchipuka urudi tena,' utakapopata ni Akili gani iliyouelekeza mti huo kufanya hivyo, nitakwambia ni Akili gani iliyoniambia kuwa mwanamke huyo alikuwa akifa kwa kansa, na akiwekewa hiyo leso, angepona."

Akasema, "Wewe siye mhubiri yule?"

Nikasema, "Naam, bwana, mimi ndiye. Mimi ni Ndugu Branham."

Akasema, "Hilo ndilo hilo jina."

79 Mzee huyo akawa Mkristo, akatoa moyo wake kwa Kristo. Mwaka jana mimi na Ndugu Wood tulishuka kule, nami nikaendesha gari tukamwone huyo mzee, naye mkewe alikuwa ameketi kwenye baraza la nyuma akimenya matofaa kutoka kwenye mti ule ule. Ndipo nikaja na kuzungumza naye, naye akasema, "Ndugu Branham, hadithi hiyo ndogo rahisi ilimwongoza yule ndugu mzee kwa Kristo, alikufa katika imani ya Kikristo mwaka mmoja uliopita."

80 Sasa, ilikuwa ni nini? Alipata njia ya Mungu iliyoandaliwa, kwa kuangalia njia ambayo Yeye angeweza kuandaa njia ya kukwepa kifo cha mti huo, alipata njia iliyoandaliwa ambayo Mungu alikuwa amemwandalia apate kuishi tena. Angalia tu njia ya Mungu iliyoandaliwa. Mungu daima hufanya njia iliyoandaliwa, katika hili lazima tuifuate.

81 Sasa, Mungu alifanya njia iliyoandaliwa kwa ajili ya jamii ya binadamu kuepuka hukumu zijazo. Katika siku za Nuhu Mungu alifanya njia iliyoandaliwa. Lakini Mungu anapofanya njia na mwanadamu anakataa kuipitia, basi kama wataikosa, si kosa la Mungu, si zaidi ya vile ni kosa la jiji unapoipita taa ya kusimama. Unaona? Amefanya njia. Naye Mungu, kabla hajauharibu ulimwengu, alijenga...alifanya safina ijengwe, isitoshe, bali Yeye alimweka nabii pamoja na Neno Lake apate kuwatengenezea watu njia ya kuepukia, na wote walioamini na kutembea katika njia ya Mungu iliyoandaliwa, na mjumbe aliyetolewa na Mungu apate kuwaelekeza kwenye njia ya Mungu iliyoandaliwa, waliepuka ghadhabu na hukumu ya mauti.

82 Mungu anaye Mjumbe usiku wa leo, aitwaye Roho Mtakatifu, Yeye ni Neno. Nalo Neno...Yeye ndiye—Yeye ndiye anayelidhihirisha Neno, lakini huna budi kuenenda katika njia hiyo. Huna budi kumsikiliza Mjumbe wa Mungu, ambaye ni Neno Lake na utembee katika njia hiyo, ni njia iliyoandaliwa, kuwa...ya kuepukia.

83 Ayubu, mojawapo ya Vitabu vya kale sana vya Biblia, kilichoandikwa, wanadai, kabla ya Mwanzo kuandikwa. Naye Ayubu, akiwa ni mtu mwenye haki, mcha Mungu, naye alijua kulikuwa na Mungu mahali fulani, naye alitaka kujua kama angeweza kuja Kwake katika siku za dhiki yake. Akasema, "Laiti ningejua mahali alipoishi, nami ningeweza kwenda

kubisha [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] mlangoni Pake na—na kuongea Naye, laiti ningepata njia, kwa namna fulani, ambayo ningeweza kumwona Mungu!"

84 Basi, Mungu alinena naye na kufanya njia iliyoandaliwa. Naye, alitaka mpatanishi, kitu ambacho kingeweza kusimama kati ya mtu mwenye dhambi na Mungu mtakatifu, na kuweka mikono yake juu ya Mungu mtakatifu, na mkono wake juu ya mtu mwenye dhambi, na kuunganisha njia kati ya hao wawili, kuleta amani. Mungu alishuka katika upepo wa kisulisuli, Ayubu akajifunga kiuno chake, Mungu alikuwa na njia iliyoandaliwa, naye Roho wa Mungu akaja juu ya huyo nabii. Alikuona kule Kuja kwa Kristo na kusema, "Najua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho atasimama juu ya nchi hii. Ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu." Amina. Mnaona? Mungu alikuwa akimwonyesha njia Yake iliyoandaliwa.

85 Ayubu 14, aliona miti, akasema, "Mti ukifa, kuna matumaini kwake kuishi tena. Lakini mwanadamu hufa, naam, huifariki dunia na kutoa roho, yuko wapi? Wanawe wanakuja kuomboleza, kumheshimu, wala yeye hajui. Laiti ungenificha kaburini, ukanilinda kwa siri mpaka ghadhabu Zako zitakapopita!"

86 Angeweza kuelewa kwamba u—ya kwamba ua lilikufa, likaishi tena; na mti ukafa, ukaishi tena; lakini akasema, "Mtu hulala chini, anatoa roho, hatumwoni akirudi tena." Aliweka mbegu ardhini, aliiona ikifa, ikioza, ikazaa uhai mwingine, lakini mwanadamu aliingia udongoni, akalala humo. Kwa hiyo, Mungu alikuwa akimfafanulia kwamba sababu ya mwanadamu kulala pale ni kwa sababu mwanadamu alikuwa ametenda dhambi na kuondoka kwenye njia ya Mungu iliyoandaliwa, njia asili, nayo njia asili ya mwanadamu kuishi ilikuwa ni kwa Neno la Mungu.

87 Mungu alilizingira Kanisa Lake kwa Neno Lake, nao walipoondoka kwenye Neno hilo, hatua moja ndogo tu yake, ilisababisha haya yote, kila maumivu ya moyo, kila huzuni, kila sikitiko, kila kaburi, kila uzee, na kila maradhi, kila ugonjwa, kila mateso yalitokea kwa sababu jamii ya binadamu ilisikiliza tu hoja badala ya Neno. Hiyo ilisababisha hilo jambo lote.

"Loo," unasema, "vema, haileti tofauti yoyote hasa."

88 Inaleta tofauti. Mungu, pamoja na Mjumbe Wake, alimwambia Lutu na mkewe, na watoto, "Hata msiangalie nyuma." Naye mke wa Lutu, huku watoto wake mwenyewe na wajukuu wake wakiungua katika hukumu za Mungu, mama, aligeuza kichwa chake kidogo tu, akaangalia nyuma, naye akalaaniwa akawa nguzo ya chumvi. Huna budi kutimiza kila Neno Lake. "Mtu hataishi kwa mkate pekee," kasema Yesu, "bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

89 Ayubu alijua basi kwamba mwanadamu alikuwa ametenda dhambi, lakini basi Mungu akamwonyesha njia Yake iliyoandaliwa inayokuja, ambapo angekuja Mtu ambaye angeweza kuweka mkono Wake juu ya mtu mwenye dhambi na Mungu mtakatifu, na kuiunganisha njia. Naye akasema, "Najua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho atasimama juu ya nchi. Ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu, ambaye nitamwona mimi mwenyewe, macho yangu yatamtazama, wala si mwingine." Haleluya! Mkombozi huyo alikuja kwa wakati mzuri kabisa.

90 Wakati wa Israeli uliwadia kwa ajili ya ukombozi, Mungu akamtoa nabii akiwa na Neno asili la ahadi, njia ya Mungu iliyoandaliwa. Sasa, Israeli walikuwa utumwani. Sasa, Musa alilikosa kwanza, alikuwa mwanajeshi, aliwazia, "Nitaenda na kuua baadhi yao, wataniogopa." Mnaona?

91 Hivyo ndivyo mwanadamu sikuzote anavyojaribu kufanya, kuchukua, kupata mafanikio yake mwenyewe, lakini huwezi, njia tayari imetengenezwa, Mungu ameitayarisha hiyo njia. Mnaona? Haidhuru ni Myahudi gani mkuu, mwerevu angeinuka na kusema, "Mnajua nini? Tunaweza kufua panga zetu, na tunaweza kulipiga taifa hili," hiyo haitafanya kazi kamwe. Mungu alikuwa na njia ya kufanya jambo hilo, na Mungu alikuwa amewaahidi ya kwamba angefanya hivyo.

92 Ndipo, wakati Mungu alipomtuma mtu huko chini, nabii, ambaye anajiliwa na Neno, alikuwa na Neno asili la Mungu, "Nimesikia kuugua kwa watu wangu na ninakumbuka ahadi yangu," (Haleluya!) kwamba Mungu habadiliki, Yeye hudumu na hilo Neno, herufi kwa herufi. Isitoshe, bali Yeye alikuwa amemthibitisha nabii Wake, alishuka, alikuwa na Nguzo ya Moto juu yake, akamthibitisha. Yeye alikuwa nanii wa Mungu. . . Huyo alikuwa ni Mungu akithibitisha ya kwamba mtu huyo alikuwa sahihi, kwa sababu alishika Neno kabisa. Loo, jamani! Alihubiri Neno, Mungu alifanya kazi pamoja naye, akiyathibitisha hayo Maneno kwa ishara zilizofuata. Yale hasa Mungu aliyomwambia Musa afanye, Musa aliyafanya.

93 Musa alikuwa na waigaji wengi, lakini katika kila hali Mungu daima alipanda wimbi juu ya waigaji wote na kulitoa sawasawa. Yesu alisema. . . Biblia inasema kwamba, "Katika siku za mwisho kama Yambre na Yane walivyompinga Musa, vivyo hivyo watu watasimama katika siku za mwisho," uigaji, iliahidi hilo.

94 Lakini, Musa alipoitupa fimbo yake chini, nao jamaa hawa huku wamesimama pale na utambuzi wa ufahamu usio wa kawaida walitupa fimbo zao chini, wakafanya jambo lile lile alilofanya Musa, ila tu, Musa alikuwa akifuata mkondo wa Mungu (Basi nini kilitukia? Hakuna kitu ambacho huyo

mtu angeweza kufanya, alikuwa ametimiza wajibu wake. Unapofanya kila kitu unachoweza kufanya kwenye wajibu, basi ni jukumu la Mungu kuandaa njia ya . . . ? . . . Mungu atajipatia Mwenyewe dhabihu. Mnaona?) basi Musa akaitupa fimbo yake chini, naye Haruni akaitupa yake chini, zikageuka kuwa nyoka, nao hawa hapa wanakuja wenye utambuzi wa ufahamu usio wa kawaida na kutupa fimbo zao chini, nazo zikageuka, ndipo basi Musa asingeweza kufanya lolote lingine, ndiposa Mungu akaandaa njia: Fimbo zao zikala hizo zingine. Ilikuwaje kwa ile fimbo? Je, huyo nyoka alikua mkubwa, ama ilikuwaje? Loo, Mungu angali anayo njia iliyoandaliwa, Naye anaweza kufanya njia, wakati hakuna njia nyingine, Yeye ndiye njia! Amina.

95 Wakati Wamisri wasingeamini ishara hizo ambazo Musa alizifanya, wasingesadiki hilo, basi ilisababisha mauti. Na wakati mtu haliamini Neno la Mungu, daima inamtenganisha na Mungu. Hawa alipokosa kuliamini Neno la Mungu ilimtenganisha yeye na Adamu kutoka kwa Mungu, maana hao wawili walikuwa mmoja. Angalia, mtu yeyote asipoliamini Neno la Mungu, Neno la Mungu ni Njia ya Mungu iliyoandaliwa, hakuna mtu anayepaswa kuongeza lolote Kwake wala kuondoa lolote kutoka Kwake, halina budi kuwa jinsi tu lilivyoandikwa, sasa, mtu yeyote anapoondoa kutoka Kwake ama kuongeza Kwake, mbona, anajitenga na Mungu, ametengwa basi.

96 Wamisri hawakuiamini ishara ya nabii yule ambayo alishuka huko na kuifanya mbele yao wote, sasa, sasa, yeye ni . . . hilo linasababisha mauti, mauti ni utengano. Basi mauti yalipokuwa tayari kupiga, Mungu aliweka utaratibu wa kuwatenganisha waaminio na wasioamini, na huo ulikuwa ni kwa damu. Damu ilifanya utengano. Yule aliyeamini kweli alikuja chini ya damu, wale ambao hawakuamini hawakukaa chini ya damu.

97 Na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, waaminio hukaa chini ya Damu. Hiyo ni kweli. Ndipo mahali pekee pa kukaa kwa usalama. Vema. Damu ilisababisha utengano kati ya mwaminio na asiyeamini kwa sababu Damu huubeba Uzima. Damu, Uhai uko katika Damu, kwa hiyo Uhai . . . Damu iko katika Uhai, naye mwaminio hukaa katika ile Damu, ambayo humletea Uzima wa Milele, naye asiyeamini huchukua kanuni yake ya imani na kuendelea mbele. Hiyo ni kweli. Hakuna njia ya kuiondokea. Vema.

98 Baada ya Musa kuwatoa nje, alifika kwenye Bahari ya Shamu, moja kwa moja kwenye wajibu, hapo Bahari ya Shamu ikawakatilia mbali. Musa alihitaji daraja, Mungu akaleta upepo. Amina. Kwa hiyo, Musa hakuninii . . . asingalilitumia hilo daraja, alichukua njia ya Mungu iliyoandaliwa, naye akasonga mbele kuelekea baharini, nayo ikafunguka, naye Musa na Israeli wakavuka juu ya nchi kavu, kwa maana walifuata njia ya Mungu iliyoandaliwa.

99 Kupitia jangwani wakaja, ile safari, huzuni kubwa na majonzi walipokuwa wakipitia. Musa akazeeka, umri wa miaka mia moja na ishirini, ndipo siku moja ikawa anaenda kufa, basi akapanda juu ya kilele cha Mlima Pisga. Ndipo alipokuwa huko juu akiitazama nchi ya ahadi, mauti ikampata, nabii huyo mwaminifu wa Mungu, wakati hapajapata kuwa na mtu aliyeishi kama yeye, lakini mauti ilimpata, nayo mauti ilipompata, alihitaji mahali angaliweza kufia, Mungu akaleta mwamba, mwamba ule ule ambao ulikuwa umemfuata nyikani, akapanda juu ya huo mwamba akafa. Ndipo akahitaji wabeba jeneza wamzike, naye Mungu akaleta Malaika, nao wakaja na kumchukua hadi mahali fulani. . .?. . .Ilikuwa ni nini? Mungu! Ikiwa tutatembea katika njia ya Mungu iliyoandaliwa, Mungu ataleta kila kitu tunachohitaji. Mungu huleta, haijalishi hali ya mambo ikoje, Yeye huleta.

100 Henoko, siku moja, ambaye alikuwa ametembea miaka mia tano mbele za Mungu, naye alikuwa na ushuhuda kwamba alimpendeza Yeye (Amina. Ni ushuhuda wa jinsi gani!), miaka mia tano na alikuwa na ushuhuda alimpendeza Mungu, basi siku moja akaanza kufanya matembezi ya alasiri, naye alihitaji njia, ndipo Mungu akampa njia kuu, naye akaondoka hapa moja kwa moja, moja kwa moja akapanda ngazi ya Yakobo, ama, barabara kuu, akipanda kwenda Nyumbani. Mnaona? Mungu alimwandalia njia ya kwenda Nyumbani. Kweli.

101 Eliya, baada ya kumkemea Yezebeli sana. . .Tunahitaji mwingine siku hizi. Hiyo ni kweli. Alimkemea sana. . .Jinsi ninii. . .Tunahitaji mmoja siku hizi. Jinsi ambavyo watu. . .Loo, ni fedheha, kwa yale watu wafanyayo siku hizi, ni ninii tu. . . na wote wanajiita Wakristo. Na baadhi ya mitindo hii ambayo wanawake wetu wa kisasa wamevaa, baadhi ya wanawake hawa wenye mtindo wa kukata nywele kichwamaji, mwajua. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

102 Nimeona ukoma, lakini sijawahi kuona chochote kama hicho. Mwanamke huyo alikuwa na macho mekundu na ya samawati, rangi ya hudhurungi kote usoni mwake, mmoja wa hao waliokata nywele mtindo wa kichwamaji. Nilimhurumia sana, nilikuwa niende huko na kusema, "Dada, kunradhi. Una tatizo gani? Mimi ni mmishenari. Unataka nikuombee? Mimi huwaombea wagonjwa." Ndipo nilipokuwa nikimwendea huyo mwanamke, wengine wawili au watatu wakatokea vile vile, nikawazia, "Masalale, hakika haiwezi kuwa mbaya hivyo." Ya kutisha. Loo, jamani, jamani, jamani! Ni fedheha jinsi gani! Naam.

103 Naye Eliya alikuwa amewakemea sana hao mama wa taifa wa nchi, na kadhalika, naye alikuwa amechoka na kudhoofika, alikuwa anaenda Nyumbani. Haleluya! Alivuka Yordani, naye alihitaji ngazi, lakini Mungu akampelekea farasi wa moto na magari ya moto. Alikuwa na. . .Mungu alikuwa na njia

iliyoandaliwa ya kumtwaa nabii Wake mzee, aliyechoka kutoka humo. Nina furaha sana kwamba Yeye angali anadumu Mungu.

104 Yoshua, baada ya kifo cha Musa, alishuka kwenye mto Yordani, alihitaji daraja, pia, apate kuvuka, lakini Mungu akampa nguvu, Roho iliyousimamisha huo mto, na kuushikilia kule juu milimani mpaka wakavuka katika nchi kavu. Mungu asifiwe.

105 Danieli, moja kwa moja kwenye wajibu, akisimama pale kama nabii mbele za Mungu, akinena Neno la Mungu, na kukataa kusujudia kitu kingine chochote, moja kwa moja kwenye wajibu wake, alitupwa katika tundu la simba pamoja na simba wenye njaa na hasira. Alihitaji mpatanishi, alihitaji ua wa kumkinga na hao simba, bali Mungu akamtuma Malaika, njia ya Mungu iliyoandaliwa kwa ajili yake. Danieli alitaka ua labda, lakini Mungu akatuma si-. . .akamtuma Malaika ambaye alimwandalia njia. Jinsi Mungu alivyo wa ajabu, kama tukitembea tu katika njia Yake iliyoandaliwa!

106 Wana wa Kiebrania walihitaji bomba, bomba la moto, huko chini katika tanuru ya moto siku moja, pia wakisimama waaminifu, moja kwa moja kwenye wajibu wao. Walihitaji bomba la kuzima huo moto, lakini Mungu akawatumia Mtu wa nne, ikamshtua sana mfalme, njia ya Mungu iliyoandaliwa.

107 Wale mamajusi kutoka mashariki walikuwa wakitazamia ile Nyota ya Yakobo izuke. Walikuwa wakitafuta kiongozi wa kuwapeleka Kwake, nao walitaka kiongozi, ndipo Mungu akawapelekea nyota, akawaongoza moja kwa moja hadi kwa yule Mfalme mchanga.

Ninaweza kumsikia mke wa Belzari akisema, “Aisee, Belzari, unaenda wapi?”

108 “Ninaenda mpaka Yerusalemu.” Loo, jamani! Hiyo ilikuwa mashariki, huko nyuma kabisa India. Nilikuwa huko hivi majuzi, bado wanakaa vile vile, wale mamajusi mitaani watatu-watatu. Basi, akasema, “Ninaondoka.” Vema, walipaswa kuwa na dira ya kuwaongoza.

Unasema, “Naam, hapa, umesahau dira yako.”

109 “Siichukui wakati huu, ninaenda kwa njia iliyoandaliwa na Mungu.” Amina. “Ninaenda kwa njia iliyoandaliwa.” Ikamwongoza moja kwa moja hadi kwa Mfalme mchanga aliyezaliwa.

110 Siku moja ulimwengu ulitaka Mwokozi, walihitaji Mwokozi, Mungu akamtoa Mwanawe, Yesu, Mwokozi, akafanyika Dhabihu; Alikuwa Mpatanishi, alipaswa kusimama kati ya mwenye dhambi na adhabu ambayo Mungu alikuwa ameweka juu yake, kusimama kati ya mauti na uzima, kuzimu na Mbinguni, Yeye alikuwa ni Mpatanishi wa Mungu, Mwokozi.

111 Baada ya kufa, kuzikwa, na kufufuka tena, Kanisa lilihitaji nguvu za kuihubiri Injili Yake. Sasa, Yeye hakuwapa elimu, Yeye hakuwajengea shule, Yeye hakuwaundia dhehebu, bali aliwapa Roho Mtakatifu, hiyo ilikuwa ndiyo njia ya Mungu iliyoandaliwa. Mungu anayo njia iliyoandaliwa, tunajaribu kuandaa njia fulani nyingine, lakini Mungu anayo njia iliyoandaliwa, sikuzote ni bora kufuata njia Yake.

"Utapokea nguvu ukiisha kupata Shahada yako ya Sanaa. Utapokea nguvu baada ya kuwa shemasi."

112 "Mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu, Roho Mtakatifu. Ndipo mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, Uyahudi," na Victoria, "na hata miisho ya dunia." Naam, bwana.

113 Baada ya miaka elfu mbili ya kutokuamini, na kuanguka, na kanuni za imani, na mafundisho, na mafundisho ya sharti yakiongezwa kanisani, walihitaji ishara wapate kujua kama bado Yu hai au la. Loo, jamani! Mungu alikuwa na njia iliyoandaliwa, thibitisho la kufufuka Kwake, ishara ambayo alikuwa amemwahidia Uzao wa kifalme wa Ibrahimu. Alimwahidi Uzao wa kifalme wa Ibrahimu kwamba ishara ile ile ambayo Ibrahimu aliona, kama tulivyolichukua jana usiku, Uzao wake wa kifalme utaona ishara iyo hiyo, nasi tunaishi katika wakati wa jioni wakati nabii aliposema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni."

114 Ni nini? Ustaarabu umesafiri pamoja na jua, ustaarabu wa kale sana tulio nao ni India, au, la, namaanisha Uchina, halafu ustaarabu umesafiri pamoja na jua, pia angalieni, na umekuja mpaka tumefika kwenye Pwani ya Magharibi. Sasa, hawawezi kwenda mbele zaidi, kama wakienda, wanarudi mashariki tena. Basi angalieni, "Siku inakuja," akasema nabii, "ambayo isingeitwa usiku wala mchana." Ilikuwa siku yenye utusitusi, yenye ukungu, mnaipata hapa pwani, mna mwanga wa kutosha mnaweza kuona jinsi ya kwenda huku na huko, lakini si kama nuru ya asili, jua linalochomoza asubuhi isiyo na mawingu.

115 Na kama vile j-u-a linavyochomoza mashariki na kutua magharibi, Injili ya M-w-a-n-a ilichomoza mashariki na inatua magharibi, na sasa jua lile lile linalochomoza mashariki, j-u-a, ndilo jua lile lile linalotua magharibi, na M-w-a-n-a yeye yule (Haleluya!) ambaye, alitupa Nuru Yake ya Injili, na nguvu, na ishara Yake ya Kimasihi kwa watu wa mashariki, katika siku za mwisho sasa mawingu yameondoka tena kutoka kwenye Kanisa, naye M-w-a-n-a anazuka akiwa na uponyaji katika mbawa Zake, na kuleta nguvu, ushahidi wa kufufuka Kwake, ya kwamba Yeye angali Mwana wa Mungu. "Itakuwa Nuru wakati wa jioni," Njia ya Mungu iliyoandaliwa, naam.

116 Mungu ameandaa njia Yake, ishara ya Kimasihi, ili kuthibitisha kwamba Yeye, kulingana na Waebrania 13:8, "Ni

Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele," njia Yake ile ile iliyoandaliwa aliyokuwa nayo kwa ajili ya Ibrahimu, ndiyo njia ile ile iliyoandaliwa aliyokuwa nayo kwa ajili ya uzao asili wa Ibrahimu, njia ile ile iliyoandaliwa aliyo nayo kwa ajili ya Uzao wa kifalme wa Ibrahamu.

117 Tunaishi katika siku za mwisho wakati makanisa yamekuwa baridi, na kanuni za imani, na mafundisho ya sharti, nao watu wamekuwa baridi, uamsho umekwisha, na watu wakirudi kwenye kila namna ya maisha. Hawataki kwenda kanisani tena, wanabaki nyumbani wakiangalia televisheni, wanatoka nje, nao wanawake wanavaa nguo wakijaribu kuiga Hollywood. Nao wanaume, wanaopaswa kuwa watawala wa nyumba zao wenyewe, wanawaruhusu wake zao kuvaa kaptura na kuvuta sigara, na kujiita Wakristo, na kuimba katika kwaya na mambo kama hayo, wakati kitu hicho chote kimejaa uchafu na matapiko.

118 Lakini Mungu alisema, "Nitarudisha miaka yote iliyoliwa na tunutu na parare na wadudu wengine wote. Nitarudisha," asema Bwana. Kanisa lile lile lililokuwa huko ng'ambo kwenye siku ya Pentekoste ambalo lilishuka, na kujaza kanisa, ambalo kanisa la Kirumi hatimaye, parare wakaunda mashirika, madhehebu, wakaula mpaka kwenye kisiki, lakini Mungu alisema angeurudisha katika siku za mwisho.

119 Nuru ya jioni itaangaza. Tunahitaji uinjilisti wa wakati wa jioni, pamoja na Ujumbe wa wakati wa jioni, sio lundo la kanuni za imani. Walikuwa na mvua ya vuli na ya masika. Neno la Kiebrania la *vuli* linamaanisha "mvua ya kupanda," halafu mvua ya kuvuna. Kupanda, tumepata nini kutokana na uamsho huu? Wafuasi zaidi. Tulipanda nini? Mbegu ya kimadhehebu; tukavuna mazao ya kimadhehebu.

120 Wabaptisti walikuwa na wito mkubwa, "Milioni moja zaidi katika mwaka wa '44." Billy Graham, mwamshaji mkuu, hiyo ni kweli, tunawathamini watu hao, lakini tunachohitaji siku hizi, ndugu, ni kupanda Mbegu ya Injili ya Neno la nguvu, ufufuo wa Kristo, Kiumbe hai anayeishi pamoja nasi, ndani yetu sasa, wakati uliopo. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Amina.

121 Tumeahidiwa mjumbe katika siku za mwisho, Malaki 4 ilisema, ambaye atarudisha imani ya watoto iwaelekee baba zao. Watoto wa Kipentekoste sasa, ambao wanajitenga nayo, atawarudisha kwenye Ujumbe wa asili wa Pentekoste ya asili. Haleluya! Najisikia kubarikiwa. Amina. Amina. "Nitarudisha." Mungu anayo njia iliyoandaliwa leo hii, ni Pentekoste iliyorudishwa, kurudi kwenye mambo yale yale, ishara zile zile, Ujumbe ule ule. Amina. Haya basi.

122 Ninasema nini? Njia ya Mungu iliyoandaliwa, tembea katika njia ya Mungu iliyoandaliwa. Ametupatia Mjumbe, Roho

Mtakatifu; ametupatia Neno, na kama roho yoyote ikinena kinyume na hilo Neno haiwezi kuwa ni Roho Mtakatifu, maana Roho Mtakatifu aliandika hilo Neno, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Waebrania 4:12, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili," hukatilia mbali nyama yote ya kilimwengu kutoka kwako, "na ni Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo."

123 "Nitarudisha," asema Bwana. "Njia, njia kuu na njia, nayo itaitwa njia ya utakatifu, wasio haki hawatatembea ndani yake." Haleluya! Huwezi kutembea na Hollywood na Kanisa wakati ule ule; huwezi kutembea pamoja na Mungu na ulimwengu wakati ule ule; huwezi kumpenda Mungu na mwanadamu wakati mmoja.

124 Tunachohitaji leo hii sio shirika zaidi, uanachama zaidi, lakini tunahitaji Kanisa kusafishwa tangu mimbarini hata kwa bawabu, na uamsho mzuri wa mtindo wa kale wa Mtakatifu Paulo, na Roho Mtakatifu wa Biblia, na watu warudi wakitembea katika njia ya Mungu iliyoandaliwa. Amina. Mungu anayo njia iliyoandaliwa, na tutembee ndani yake.

125 Mungu aliahidi alipokuwa hapa duniani, Yeye aliahidi, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya," Yesu aliahidi hapo awali, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu." Ni nini? Njia ya Mungu iliyoandaliwa.

126 Kundi la wanafunzi lilikuwa huko nje baharini siku moja. Walikuwa wameuangalia mkutano mkuu siku hiyo, nao wakamwona Mtu ambaye angeweza kuumega mkate, kuukatakata, na kuuweka chini, ndipo mkate mwingine ukamea juu yake, akauweka chini hata akawalisha watu elfu tano. Jamani! Wakasema, "Huyo hana budi kuwa ni Mungu, hakuna kitu kingine ambacho kingeweza kufanya hivyo ila Mungu." Huyo hapo.

127 Walikuwa huko nje kwenye meli baharini, walikuwa wameondoka bila Huyo, wakaenda zao bila Yeye. Hao hapo, wakirushwarushwa huku na huku, wala hawakujua waende wapi, makasia yalivunjika, meli ilikuwa imejaa maji, matanga yaliraruka, wala hawakuwa na njia ya kuziondokea nguvu za Shetani zilizokuwa zikiwafokea.

128 Sijui siku hizi kama hatujayakimbilia madoido pia, katika uamsho, kujenga mahali papya, na kutawanyika na kujenga majengo mapya, makubwa, na kuhubiri ya kwamba Kuja kwa Kristo kumekaribia, matendo yetu wenyewe yanashuhudia dhidi yetu. Loo jamani, na wamishenari wasio na viatu miguuni mwao! Kuna nini, ndugu? Kuna kasoro. Angalia hali ingawa kanisa limeingia ndani yake, lakini Mungu aliahidi kutokana na hayo kwamba angerudisha, angerejesha, angefanya njia.

129 Wanafunzi hawa huko nje, matumaini yote yalikuwa yamekwisha, walikuwa tayari wamekata tamaa, kasema, "Vema, hatuwezi kwenda mbali zaidi, tutafia tu hapa kwenye bahari hii usiku wa leo." Ndipo huyo hapo Yesu akaja akitembea juu ya maji, na jambo la kuhuzunisha lilikuwa, Mungu alikuwa amewaandalia Njia ya kuepukia, nao waliiogopa, wakasema, "Inaonekana ya kutisha. Loo, yeye ni mizuka." Nao wakalia kwa hofu.

Yesu akasema, "Msiogope; furahini; Ni Mimi."

Mungu ameandaa njia kwa ajili ya watu siku hizi waone ya kwamba tunaishi katika wakati wa mwisho, msiogope jambo hilo, aminini.

130 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu sasa. Mungu anayo njia iliyoandaliwa, marafiki, imeainishwa njiani kote, ni nyembamba, "Njia ni pana iendayo upotevuni, bali njia ni nyembamba iendayo uzimani, na ni wachache tu watakaoipata."

131 Je, wewe ni mmojawapo hapa usiku wa leo ambaye haijui njia hiyo, ambaye hajui maana ya kutembea katika njia ya Uzima, humjui Kristo, hujajazwa na Roho? Nitakuuliza, kama mtumishi Wake, kwa unyofu wa moyo wangu, kama uko hapa wala humjui kama Mwokozi wako, je, waweza kuinua mkono wako na kusema, "Ndugu Branham," ukiinua mkono wako, itakushuhudia, "Nataka uniombee ili nitembee katika njia ya Mungu iliyoandaliwa"?

132 Unaweza kuwa mshiriki wa kanisa, hilo halimaanishi kitu; angalia, unasema, "Vema, ninaishi maisha mazuri, safi," hiyo bado haimaanishi kitu kwa Mungu. Ni—ni nani angeweza kuwa safi zaidi, ni nani angeweza kunena kwa utakatifu kuliko wale Mafarisayo wa siku hizo? Walikuwa watu waaminifu ambao tungewaita watu wacha-Mungu, lakini Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu ibilisi," kwa sababu hawakumjua Masihi wao. Ikiwa humjui Yeye kibinafsi . . .

133 Tunawapeleka watoto wetu kwenye shule za Biblia na vyuoni, nasi tunawafunza Biblia. Je, kuna faida gani kuijua Biblia ikiwa humjui Mwandishi wake? Biblia haisemi kulijua Neno, Shetani anajua Neno kuliko mwanafunzi yeyote duniani, hilo halimfanyi kuokoka, sio kwa kulijua Neno, ni kumjua Yeye ni Uzima, kumjua Yeye.

134 Kama humjui, inua mkono wako, useme, "Ndugu Branham, niombee, nataka kumjua, kwa uaminifu, kwa moyo wangu wote, nataka kumjua." Je, kuna wenye dhambi hapa ambao unaweza kuinua mkono wako na kusema, "Niombee, nataka kumjua, ninataka kutembea katika njia Yake, njia ya Mungu iliyoandaliwa. Ninatambua kuwa nimejiunga na kanisa, lakini kama nilikuwa nikifa sasa hivi ningeogopa hata kufa, singeokoka"? Mungu akubariki. Je, kuna mwingine? "Nataka

kumjua Yeye." Mungu akubariki, ewe msichana. Mungu akubariki. Mungu akubariki, mama. Hilo ni jema.

135 Ndugu Brent, Mungu akubariki, bwana. Ninakwambia, inahitaji mwanamume halisi kukubali kuwa amekosea, anapokosea, atakubali, nina matumaini mengi kwa mtu huyo; wakati mwanamke amekosea na atakubali, nina matumaini mengi kwa ajili yake; lakini wanapokosea wala hawatakubali: "Yeye afichaye dhambi yake, au, afunikaye dhambi yake, hatafanikiwa, yeye anayeungama dhambi yake atapata rehema." Kama umekosea na unajua, inua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham." Mungu akubariki, ndugu. Mwingine, kabla tu ya maombi? Mungu akubariki, mama. Naam, Mungu akubariki hapa, na wewe, mama. Mungu akubariki. Huo ni—huo ni ujasiri halisi kufanya hivyo.

136 Sema, "Naam, Bwana, ninaamini." Ninaangalia tu mikono, Yeye pia anaangalia. Usiwe na shaka, amini tu. Endelea tu kuomba, ukiangalia . . .?. . . Acha iwe . . . Litafakari kabisa sasa, kama ulikuwa unakufa. Hivi wewe, una hakika umeamua, uamuzi wako ni mzuri?

137 Baba yetu wa Mbinguni, kumekuwa na mikono kumi na mitano au zaidi iliyoinuliwa, nijuavyo mimi, wao ni wahitaji, Bwana, wako tayari kuinua mikono yao na kusema kwamba "Nimekosea, niombee."

138 Bwana Mungu, nitakunukulia Maneno Yako, Wewe ulisema katika Injili ya Yohana Mtakatifu mlango wa 5 na kifungu cha 24, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hiyo ilikuwa ahadi Yako, Bwana.

139 Sasa, waliinua mikono yao, wakionyesha ya kwamba kulikuwa na Roho fulani karibu nao, roho wao, akiwaambia kwamba wamekosea, nao wakainua mikono yao kwa Muumba aliyewaumba, ili watambulishe Kwake kwamba walikuwa wamekosea. Baba, kutoka katika vilindi vya mioyo yao, kama hilo lilisemwa, walipita kutoka mautini kuingia Uzimani, Wewe uliahidi hilo, ulisema, "Yeye atakayenikiri mbele ya watu, nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu."

140 Kuna Dhabihu iliyotolewa, Mungu ameitoa kwa ajili ya magonjwa yetu, kwa ajili ya wokovu wetu, kwa yote tunayohitaji, Mungu anayo njia iliyoandaliwa; Yeye ni Yehova-Yire, "Bwana anaweza kujipatia Mwenyewe dhabihu," Naye alifanya hivyo. Amani na rehema Zako na zikae juu yao, Baba. Wao ni Wako, ndio Yesu amekupa Wewe, Yeye alisema, "Hakuna mtu anayeweza kuwatoa mikononi Mwake." Wao ni Wako.

141 Walimaanisha hilo, naamini, Mungu, kwa moyo wangu wote walimaanisha, nami ninaomba maombi haya ya imani kwa ajili yao wapate kujua ya kuwa Wewe ndiwe Mungu, ya

kwamba hujafa, ya kwamba ulikufa wakati mmoja, ukafufuka siku ya tatu. Na miaka elfu mbili ya ukosoaji, na—na kila njia ulimwenguni ya kulichafulia Jina Lako, na kuifutilia mbali Biblia, Lingali linasimama leo, Nawe umesimama ukilishuhudia. “Amin, mimi ni hai hata milele, na ninazo funguo za mauti na kuzimu,” akasema Mwokozi wetu.

142 Sasa, Bwana, hao ni Wako, mbele ya umati huu, na jeshi hili la Mbinguni, na Kanisa la Mungu aliye hai, ni Wako. Wahifadhi, Baba, na katika siku hiyo kuu, jalia tupate majaliwa ya kukutana sisi kwa sisi tena kuizunguka meza ile ya ushirika kwenye jioni ile ya Meza ya Bwana, kwenye ule Ufalme tena, pamoja Naye. Jalia wapate kanisa zuri, kanisa zuri la Full Gospel, wabatizwe katika ubatizo wa Kikristo, na kisha, Baba, wampokee Roho Mtakatifu na kuishi maisha ya utauwa baada ya hapa. Tujalie, katika Jina la Yesu. Amina.

143 Sasa, kabla tu sijawaomba mje hapa na kusimama hapa karibu kwa ajili ya maombi, ni wagonjwa wangapi hapa ndani, ama watu ambao wana haja na Mungu, hamna kadi za maombi? Inua mkono wako, unaona.

144 Ikiwa Neno limehubiriwa, naye Bwana akathibitisha Neno lililohubiriwa, akifanya miujiza na ishara. . .Sasa, jana usiku nilipitia. . .kuwaonyesha ya kwamba Yesu, kile ishara Yake ilikuwa kama Masihi, nikakishusha kupitia siku za Ibrahimu, na kuwaonyesha kiliumalizia muda wa wakati wa Kiyahudi, kikamalizia pale pamoja na Ibrahimu katika wakati wake, kiliahidiwa na Yesu kwa Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, ambao ni Kanisa, na kwenye wakati Wao; nikawaambia kwamba Mungu hawezi kamwe kufanya uamuzi, na akiitwa jukwaani kufanya lolote, hana budi milele kulifanya kwa njia ile ile. Mungu alipoitwa kumwokoa mtu, kama angesema, “Asimame kwa kichwa chake,” ilibidi iwe hivyo milele. Mungu alimwokoa mtu kwa damu iliyomwagika ya mtu asiye na hatia, na daima imebaki vile vile.

145 Tumejaribu elimu, madhehebu, kila namna ya mipango, na zote zinashindwa na kupeleka watu mbali zaidi na Mungu na mmoja kwa mwingine, lakini tunapokuja chini ya Damu iliyomwagika, Methodisti, Baptisti, Katoliki, Presbiteri, na wote tunaweza kukubaliana, kwa sababu tuko katika njia ya Mungu iliyoandaliwa, ushirika kwa Damu ya Yesu Kristo, misingi pekee ya pamoja ya ibada iliyoko katika ushirika. Hatujali kama watawala, mahakimu, chochote kile, wameketi karibu wakati Roho anaposhuka, tuko hapo kumwabudu Mungu, kwa sababu hatuionei aibu Injili ya Yesu Kristo, kwa maana ni uweza wa Mungu uletao wokovu, Njia ya Mungu iliyoandaliwa kwa ajili ya mwenye dhambi.

146 Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Ninyi nyote hapa mmekuwa kwenye

mikutano hapo awali, na mnajua ninachotaka kufanya. Sasa, ninabashiri hili, ya kwamba Kanisa liko katika hali mbaya sana liliyopata kuwa ndani.

147 Wale watumwa wa Misri hawakujua, waliposimama ukingoni baada ya kuona uamsho mkubwa ambao nabii huyo alishuka na kuwaletea, nao walikuwa wameuona mkono wa Mungu wenye nguvu, nao walikuwa wamelindwa na kuja huko nje, na kucheza katika Roho baada ya kuvuka Bahari ya Shamu na kuona adui zao wakizama nyuma yao, tabia zao zote, na kadhalika, kama tunavyoweza kusema leo, zilizama nyuma yao, mambo yanayowatesa, huku Miriamu akicheza katika Roho, na Musa akiimba katika Roho, na kadhalika, kamwe hawakujua kwamba walipokuwa na takriban siku kumi tu kutoka kwenye nchi ya ahadi, wakijua ya kuwa walikuwa umbali wa miaka arobaini kutoka kwake. Kwa nini? Kwa sababu walikataa kumfuata Mungu, walitaka sheria badala ya neema, nao wakaipata, ili waweze kujitengenezea njia yao wenyewe na kuwa na *hiki-na-hiki* chao wenyewe, mwanadamu sikuzote amejaribu kufanya jambo fulani mwenyewe, ndipo Mungu akamwacha kila mmoja wao aangamie nyikani, na kuinua kizazi kipya na kuwapeleka kwenye nchi ya ahadi.

148 Kanisa la Kipentekoste halikujua, miaka arobaini ama hamsini iliyopita, mlipokuwa mkicheza katika Roho, hao akina mama wenye nywele ndefu waliovaa nguo ndefu, kwamba binti zao wangepata kuwa malkia wa Hollywood, kama wanavyojaribu kuwa siku hizi; hawakujua, wakati watu waadilifu, na watu watauwa ambao wangekufa kwa ajili ya Neno hilo, wasimame chini ya milio ya risasi na chochote kile, wakaitwa "mtakatifu anayebingirisha," wakatupwa gerezani, wakasimama pembeni mwa barabara, wakitoroka kona moja, wawe kwenye ile nyingine, wakileta Injili, kwamba wana wao wangeruhusu jambo kama hilo lije, kuyafikisha makanisa yenu mahali fulani kama madhehebu mengine. Sasa wanatangatanga, kwa miaka arobaini wamekuwa wakitangatanga, lakini kuna jipya linalokuja, "Mungu atarejesha," asema Mungu, mtu ambaye atatembea katika Roho, ailete ile Kweli, na kusema ukweli. Yoshua, Yehova-Mwokozi, aliwaongoza kuuvuka Yordani.

149 Sasa, ndugu, dada, Kristo yu hai leo, hajafa, kama amekufa, basi dini yetu ni bure. Alifufuka tena, yu hai hata milele, alifanyika tu mauti kwa maana angeweza kuondoa dhambi, ilikuwa ni Imanueli.

150 Alipoupanda ule mlima, yule nyuki wa mauti akivuma pande zote, akijua atamwuma, hawakufikiri kwamba Yeye alikuwa, Shetani hakuamini Yeye alikuwa ni nabii. Mbona, dhihaka hiyo, wakaweka kitambaa usoni Mwake, na kumtemea mate usoni, na kumpiga kichwani kwa mwanzi, na kusema, "Ikiwa wewe ni nabii, twambie ni nani aliyekupiga." Mnaona?

"Ikiwa wewe ndiwe Mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate." Unaona? Maskini Farisayo aliyesimama pale akasema, "Kama angekuwa nabii, angejua ni mwanamke wa namna gani aliyekuwa anaosha miguu yake," kana kwamba hakujua. Mnaona?

151 Alipomwona Simoni na kumwita jina lake, na kumwambia, "Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona," hiyo Mbegu ya Mungu iliyochaguliwa tangu zamani ikahuishwa upesi namna hiyo. Wakati Filipo alipoenda akamkuta Nathanaeli na kumleta pale, Yeye alisema, "Tazama Mwisraeli kweli kweli, ambaye hamna hila ndani yake!"

Akasema, "Rabi, ulinijua lini Wewe?"

Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikujua."

152 Akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli." Walijua hiyo ilikuwa ni ishara ya Kimasihi. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo ilikuwa njia ya Mungu iliyoandaliwa kwao kumwona.

153 Yule Malaika kule chini Sodoma, aliyegeuza mgongo Wake kuelekea kwenye hema, na kumwuliza Ibrahimu alikuwa wapi Sara, mkewe, naye alikuwa hemani, ndipo Yeye akasema, "Nitakurudia kulingana na uhai," naye Sara akacheka moyoni mwake, akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" nyuma Yake, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu," Ibrahimu alipitia kila namna ya ishara na kadhalika, lakini kabla tu ya ule moto ikaja ishara hiyo.

154 Israeli walipitia ishara za kila namna, lakini kabla hawajatengwa na Uwepo wa Mungu, waliiona hiyo ishara ya Kimasihi. Kanisa limeshuka kupitia Lutheri, Baptisti, Presbiteri, kote kupitia Pilgrim Holiness, na Wanazarayo, Wapentekoste, kufikia kunena kwa lugha, lakini Hii hapa, wana ninii . . . jambo fulani halina budi kutokea, Yeye hana budi kuwa Mungu yeye yule.

155 Sina elimu, mimi ni ndugu yenu, lakini ninawaambia Kweli, na kama ninawaambia Kweli, Mungu hana budi kuiunga mkono Kweli hiyo, na iwapo si Kweli, Mungu hatakuwa na uhusiano wowote nayo. Hiyo ni . . .

156 Nyinyi nyote . . . Sote tunajua Neno la Bwana liliwajia manabii, manabii walikuwa ni Neno la Bwana lililodhihirishwa. Yesu alikuwa Nabii, na hiyo ndiyo sababu Kumbukumbu la Torati ilisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii," nao walipomwona akifanya hivyo, hawakuwa na nabii kwa mamia ya miaka, lakini walijua Huyo alikuwa ni *yule* Nabii.

157 Mwangalie maskini mwanamke yule mzee huko juu, kahaba, katika Yohana Mtakatifu 4, aliposimama pale siku hiyo,

Yesu akatokea, Myahudi, akamwomba maji, nayo mazungumzo yakaendelea kwa muda mrefu, Yesu alikuwa akijaribu kujua ilipokuwa shida yake, ndipo alipopata ilipokuwa shida yake, akasema, "Nenda, kamwite mume wako mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume."

Akasema, "Kweli, ulikuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako."

Mwangalieni maskini mwanamke huyo, akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ndiwe *yule* Nabii."

158 Sasa, mkiangalia, King James inasema "nabii," lakini fuatilia maandishi ya pambizoni, "*yule* Nabii" aliyekuwa aje. Walimwuliza Yohana, "Je, wewe ndiye *yule* Nabii?" Walijua ya kwamba Masihi huyo alikuwa awe Nabii.

159 Akasema, "Je, Wewe ndiwe *yule* Nabii ajaye? Tunajua wakati Masihi, anayeitwa Kristo, ajapo, hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake, Yeye atatuonyesha mambo haya, lakini u Nani Wewe?"

Yesu akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye."

Ndugu, hao Mafarisayo, walioelimika kweli kweli, wa kimadhehebu, walisaga meno, wakasimama pale na kusema, "Ni ibilisi, Beelzebuli, mpiga ramli."

160 Yeye akasema, "Nimewasamehe; lakini siku moja Roho Mtakatifu atakuja kufanya jambo lilo hilo, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao." Akasema, "Yachunguzeni Maandiko, Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Alikuwa Neno la Mungu lililofanyika mwili, Yeye ni Dhihirisho. "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, msiniamini Mimi; Maandiko yananishuhudia Mimi, mnadhani ndani Yake mnao Uzima wa Milele, Hayo yananishuhudia Mimi." Kwa maneno mengine, "Ndiyo Mambo yale yale hasa yanayosema kile nilicho Mimi."

161 Sasa, Maandiko yale yale yanasema siku tunayoishi, yakithibitisha ya kwamba tuko katika wakati wa jioni, naye Mungu amefanya Njia ya kuepukia, ikimbilieni upesi mwezavyo, huko Kuepukia ni Yesu Kristo, Roho Mtakatifu, kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Huo.

162 Wala, msitegemee, ninaamini katika kupaza sauti, kunena kwa lugha na hayo yote, lakini msitegemee hayo, ni Uzima uliomo ndani yake, na Uzima huo ndio unaoamini Neno hilo, haijalishi kama ulinena kwa lugha, na lolote ulilofanya, na bado unatilia shaka Neno hilo, aliye ndani yako si Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu aliliandika hilo Neno, wala Roho Mtakatifu hawezi kulikana Neno Lake Mwenyewe. Mnaona? Roho Mtakatifu ataitikia kila moja ya sentensi hizo kwa "Amina. Amina," sawasawa kabisa, mstari juu ya mstari, mstari juu ya mstari, Roho Mtakatifu ataitikia.

163 Naye Roho Mtakatifu Ndiye aliyetoa ahadi. Mtu yeyote anajua ya kwamba Biblia ilisema kwamba "Yesu Kristo, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Mtu yeyote anajua ya kwamba Biblia ilisema, Waebrania 13:8, ya kwamba "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele." Kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, hana budi kutenda vivyo hivyo kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule. Yesu alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya." Alifanya kazi za aina gani?

164 Biblia inaonyesha waziwazi kwamba tuko katika siku ya mwisho na ishara ya mwisho. Mimi ni mdogo kiasi bado, nina umri wa miaka hamsini na mitatu. Tazameni hili, katika Jina la Bwana, kamwe hamtaona lililo kuu zaidi, najua mnatazamia kitu fulani kikuu, lakini angalieni, umeweka jicho lako... uko kwenye njia mbaya papo hapo. Hebu someni milango mitatu ya kwanza ya Ufunuo, hakukuwa mambo mengi sana yaliyoahidiwa Kanisa la Mataifa. Hiyo ni kweli. Mambo hayo mnayosoma, hayo yanakuja huko Israeli baada ya Kanisa kuondoka. Kwa hiyo, iweni waangalifu, ndugu, inapita moja kwa moja, wala hamjui.

165 "Ni yupi kati ya manabii ambaye baba zenu hawakumpiga mawe kwa sababu hawakujua siku yao? Kama mngalinijua Mimi mngaliijua siku Yangu." Hawakumjua Yohana mpaka alipokuwa amekufa, akazikwa; hawakumjua Yesu mpaka alipokufa, akazikwa; hawakumjua Mtakatifu Patrick; Joan wa Arc, kanisa Katoliki lilimchoma moto kama mchawi kwenye nguzo, kwa sababu mwanamke huyo alikuwa na nguvu katika maombi na aliona maono, nao wakasema alikuwa mpiga ramli, mchawi, nao wakamchoma moto mwanamke huyo, akilia kwa sauti kuu apate rehema. Loo, bila shaka, mlifanya vitubio miaka mia mbili baadaye, mkaichimbua miili ya hao makasisi na kuitupa...lakini iliwapita, nanyi hamkujua.

Hata wanafunzi walisema, "Kwa nini waandishi wanasema Eliya hana budi kuja kwanza?"

Kasema, "Eliya amekwisha kuja wala hamkumtambua." Inapita juu ya kichwa chako wala hujui, usilikose, Roho Mtakatifu, Kristo, yuko hapa.

166 Sasa, kumbukeni maneno haya mawili kabla sijawaacha, kuonekana kwa Kristo na Kuja kwa Kristo ni mambo mawili tofauti. Kristo sasa anaonekana katika utimilifu wa nguvu Zake, Kuja Kwake kutakuwa baadaye, kuonekana Kwake kunatangulia Kuja Kwake. Mungu aturehemu.

167 Sasa, kila mtu hapa na awe na kicho kabisa, nilikuwa nikizungumza, nikingojea, mpaka nilipojua Uwepo Wake ulikuwa hapa. Nitamwomba, katika Jina la Yesu Kristo, atuchukue mikononi Mwake na atuondolee kutokuamini kwetu. Zichukue hofu zangu, na mashaka, na fadhaa, Mungu, yaondoe

masumbuko ya kundi hili, upate kuzitenda kazi ulizoahidi katika siku za mwisho, tupate kuondoka hapa usiku wa leo, Mungu, huku mioyo yetu ikiwaka ndani yetu, na kuona kwamba yule Mungu ambaye tumemtumikia, ambaye tumempazia sauti, tumemsifu, Huyu hapa akijionyesha Mwenyewe hai miongoni mwetu. Tujalie, Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo, na iwe hivyo.

168 Sasa, kama kungekuwa na shaka lolote moyoni mwa mtu yeyote, wewe njoo hapa na upachukue mahali pangu, lakini kama nimesema Kweli, Mungu anawajibika kuunga mkono Ukweli huo. Sasa, wewe uliyeinua mkono wako, nitakuomba ufanye jambo fulani kwa dakika moja, lakini ninyi mnaojua na kuamini ya kwamba haya, niliyowaambia, ni Kweli, basi nyinyi ombeni na kusema, "Bwana, nijalie niguse vazi Lako kwa imani yangu usiku wa leo." Sasa, kama ukinigusa, haitafaa chochote, si zaidi ya ndugu zangu hapa, ama mtu yeyote huko nje; lakini hebu umguse Yeye wakati mmoja!

169 Mwangalie Roho, hivyo ndivyo tunavyomjua Kristo, si kwa jinsi alivyovalia, si jinsi, kama nilivyosema, alivyochana nywele Zake, ama ndevu Zake, kwa usemi Wake, lugha, bali walijua Maisha Yake; Kristo ni Maisha. "Tunajua ajapo Masihi atatwambia mambo haya. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

170 Ombeni tu, kwa uaminifu, msiwe na wasiwasi, mkifanya hivyo, hamtawahi kamwe kulishika, iweni tu rahisi. Sema tu, "Bwana . . . " Ni urahisi ambao wanapuuza, wanalifanya gumu sana mpaka wao . . . Hiyo ndiyo sababu walimkosa Yesu hapo kwanza. Kasema, "Isaya alisema vizuri, 'Mna macho, hamwezi kuona; masikio, wala hamwezi kusikia.'" Mnaona? Inakufanya utambue tu ya kwamba Kristo, Mwana wa Mungu, yu hai.

171 Sasa, wewe omba. Na kama Mungu akifanya kile ambacho Biblia inasema Yeye hufanya, basi ukweli ni kwamba, Biblia ni ya kweli, lakini kama hatafanya hivyo, basi si Mungu. Nasi tunajua jambo hilo, mtu yeyote anajua hilo, ya kwamba Mungu anawajibika kwa Neno Lake. Je, hamwamini hivyo? Hana budi kulitimiza Neno Lake. Sasa, wewe omba tu sasa na uamini kwa moyo wako wote ya kwamba Mungu atakujalia. Na sasa, na amlete Roho Wake, na aseme nasi, na kulithibitisha Neno. Sasa, angalieni kwa makini sana.

172 Sasa, kumbukeni, ni wangapi hapa ndani, mnapoomba kimya-kimya, wameiona ile picha ya yule Malaika wa Bwana kwenye karatasi hiyo? Loo naam. Hakika. Nafikiri wameionyesha humu jengoni. Kwa hiyo naomba heri, nikiwa na Biblia hii hapa, nayo ikiwa juu ya moyo wangu, katika Siku ya Hukumu nitahukumiwa nanyi mtahukumiwa endapo tutamkosa Kristo, Nuru iyo hiyo haiko futi moja kutoka mahali ninaposimama sasa hivi. Sasa, Yeye alisema, "Ninatoka kwa Mungu, tena ninaenda kwa Mungu." Nuru hiyo ilishuka na

kufanyika mwili, ilirudi kutoka kwa ufufuo ikaingia Utukufuni, naye Paulo, akienda zake Dameski, alipigwa akaangushwa Nayo. Sasa, kama Nuru hiyo, ambayo ulimwengu wa kisayansi umethibitisha ya kwamba ni Kiumbe cha Kimbinguni, kama hiyo haitoi Uzima ule ule ambao ilitoa ilipokuwa hapa katika Kristo, kama haifanyi jambo lile lile katika Kanisa Lake, basi si Uzima ule ule, kama ikilifanya, ni Uzima ule ule.

173 Hapa. Nataka . . . Angalieni hapa. Kuna maskini mwanamke aliyeketi papa hapa, ameinamisha kichwa chake chini wakati uo huo. Imani, akijaribu kuamini, anaombea macho yake, macho yake yako katika hali mbaya, anayahofia, ananitazama mimi moja kwa moja. Yeye si . . . Yeye ni . . . kutoka Norwe. Hiyo ni kweli. Je, una kadi ya maombi? Huna? Huhitaji moja, macho yako yatapona sasa hivi. Imani yako iligusa- . . .

Iweni na imani. Sasa, nataka tu—kuchukua tu muda wetu kwa dakika moja tu.

174 Nenda kwa yule mama. Simama kwa dakika moja, yeyote yule huyo mwanamke alikuwa. Alikuwa wapi? Mnaona, ni ono, ni kana kwamba niliota kitu fulani. Mwanamke huyo alikuwa wapi? Sasa, nafikiri ilikuwa moja kwa moja huko nyuma katika . . . Hapa. Je, mambo hayo yalikuwa kweli, mama, yaliyosemwa? Inua mkono wako. Hivi . . . ukiomba namna hiyo, na kadhalika? Ningejuaje alikuwa akiomba juu ya nini, na yale ninii yake . . . alichokuwa akiomba, na yote juu yake, na kwamba ni nani, na mahali alipo, na yaliyotukia, na kadhalika? Ningejuaje wakati huyo mwanamke ni mgeni kabisa kwangu? Sijawahi kumwona maishani mwangu, nasi hatufahamiani kabisa. Mwendeeni baada ya ibada mkamwulize. Asante. Alifanya nini? Hilo linayathibitisha Maandiko, "Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu."

175 Hapa, huyu hapa mtu anakuja, akija mbele yangu, kamba okozi inakuja hapa, ameketi hapa mwishoni mwa safu, akiumwa na mgongo. Je, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, pamoja na maumivu hayo ya mgongo, uliyeketi hapa? Je, unaamini kwamba Mungu atakuponya? Unaamini? Unakubali uponyaji wako? Bw. Sanders, unaamini kwamba Mungu ndiye Mponyaji mkuu? Nataka kukuuliza jambo fulani. Angalia hapa nilipo, jana jioni ulikuwa na hisia za ajabu sana ulipokuwa hapa mkutanoni, jambo fulani limetukia, sasa, usiku wa leo linapokurudia tena, sasa, amini kwa moyo wako wote, ya kwamba hiyo shida imekuondokea. Unaamini?

176 Hapa, sikujui. Hatufahamia- . . . Je, huioni Hiyo? Angalieni hapa, ndugu, angalieni *pale*, moja kwa moja juu ya mtu huyu *hapa*, Nuru ya manjano-zumaridi. Huyu mtu anateseka, yuko katika hali mbaya. Ni wasiwasi, yuko karibu kuingia kichaa, ni kichaa, hivyo tu. Wewe ni mtu mzuri, una familia, lundo la watoto, yapata watoto watano. Hiyo ni kweli. Je, una kadi

ya maombi? Huihitaji. Yote yamekwisha sasa, nenda nyumbani, kawatafutie riziki watoto wako, imani yako imekuponya.

177 Unamwona mvulana huyu aliyeketi karibu nawe? Niliponyoosha kidole changu pale, aliruka. Ikiwa utaamini, ugonjwa huo wa ngozi utakuacha pia, nawe utapata afya. Unaamini? Je, una kadi ya maombi? Huihitaji sasa, imani yako imekuponya.

178 Je, huamini kwa moyo wako wote? Waulize watu hao. Siwajui, wameketi tu hapa mkutanoni, bali wana imani.

179 Huyu hapa mama mmoja ameketi hapa akiniangalia moja kwa moja, papa hapa, anaumwa na mgongo, pia. Ataamini . . . Binti Cobbles. Sikujui wewe. Je, una kadi ya maombi? Huihitaji, imani yako imekuokoa.

180 Je, ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Hii ndiyo njia ya Mungu, itembelee. Ni nini? Yesu Kristo aliyefufuka. Sahau kanuni hizi zote za imani na mambo unayojaribu kushikilia, yaachilie. Neno linafanyika mwili miongoni mwetu, tunaona ni Neno la Mungu.

181 Mnampenda? Je, ungependa kuja kuyakabidhi maisha yako Kwake, kama maisha ya huduma, hata ibada ya kuwekwa wakfu, kuweka wakfu maisha yako Kwake tena? Je, ungefanya hivyo? Wakati tukiwa Mbele Zake, nataka kila mtu aliye hapa, ambaye anataka kuweka maisha yake wakfu upya, na ninyi watu wote mlioinua mikono yenu muda mfupi uliopita, mje msimame hapa kwa dakika moja tu. Ninajisikia kuongozwa kufanya hivi, na ninapojisikia kuongozwa, sikuzote ni jambo sahihi. Hiyo ni kweli. Loo, sasa, mtaona jambo fulani likitukia.

Naam, tutakusanyika mtoni,
Ule mto mzuri, mzuri;
Loo, tutakusanyika pamoja na watakatifu kwenye ule mto
Unaobubujika karibu na Kiti cha Enzi cha Mungu.

Naam, tuta- . . . (Sisi sote!) . . . mtoni,
Ule mto mzuri, mzuri;
Tutakusanyika pamoja na watakatifu kwenye ule mto
Unaobubujika karibu na Kiti cha Enzi cha Mungu.

Tuta . . . mtoni,
Ambapo miguu ya Malaika wanaong'aa imekanyaga,
Ambapo . . . ? . . .

Hebu tuinue mikono yetu sasa.

Naam, tutakusanyika mtoni,
Mto mzuri, mzuri;

Tutakusanyika pamoja na watakatifu kwenye ule mto
Unaobubujika kutoka kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Mpiga kinanda ataendelea na huo huku tukiuimba mioyoni mwetu. [Ndugu Branham anavumisha, *Tutakusanyika Mtoni*—Mh.]

. . . nyunyizio lake la fedha,

Endeleeni tu kuuvumisha sasa, mkiwazia mnakuja Mbele za Roho wa Mungu aliye hapa pamoja nanyi.

. . . tutakusanyika mtoni,

182 Baba wa Mbinguni, ninatembea mbele ya kundi hili lililotubu, kanisa zima ila takriban watu wapatao kumi au kumi na watano limesimama kwa miguu yao, wakitaka kukujua Wewe kwa karibu zaidi, kutembea pamoja Nawe, kukupenda zaidi. Wamesimama, Bwana, wakiimba, *Tutakusanyika Mtoni*, naam, Bwana, tutakusanyika huko, na haitachukua muda mrefu.

183 Wakati ule utakapotimia, ndipo Roho wa Mungu, aliye hapa sasa hivi, Roho Mtakatifu mkuu akizunguka juu ya hili jengo, ule utamu wa ushirika unaotuvuta karibu Naye, akitujulisha ya kwamba dhambi zetu zimesamehewa, uovu wetu umetoweka . . . Tunapokuwa tayari kukiri makosa yetu, Mungu yuko tayari kutusamehe.

184 Baba wa Mbinguni, kwa kuwa tunaona siku imeenda sana sasa, nasi tumekuona ukifanya jambo usiku wa leo kama ulilofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, hizo ni kazi zile zile ulizofanya kabla ya kusulubiwa, na hapa sasa tunajua kwa jambo hili, ahadi ya Neno, kwamba liliahidi kwamba litalifanya tena, tunajua kwamba umefufuka katika wafu na uko hai hata milele. Miaka elfu mbili ya ukosoaji na kupindwa kwa theolojia, kamwe hakujaweza kulipotosha kutoka kwa Neno la Mungu. Tunamwona Kristo akija jukwaani na kufanya jambo lile lile hasa alilofanya alipokuwa hapa duniani, tunajua kwa jambo hili ya kuwa Yeye yu hai, na tunajua kwa jambo hili kwamba tumekubalika, kwa sababu Malaika aliyekuja kwa Ibrahimu na kwa lile kundi lililoteuliwa, si kule chini Sodoma, bali juu kwenye kundi lililoteuliwa, alifanya ishara ya namna hii.

185 Basi, tunafurahi sana, Mungu, kwamba umetufahamisha ya kwamba sisi ndio lile Kanisa ambalo limetoka na kutengwa, si kule chini Babeli tena, bali wanazaliwa mara ya pili na kufanywa viumbe vipya katika Kristo Yesu, wakingojea Kuja Kwake. Hatuyajali mambo ya duniani, kwa maana sisi ni wasafiri na wageni, Urithi wetu ni wa huko juu ambapo Mungu ameketi kwenye Kiti Chake cha Enzi.

186 Tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utamchukua kila mtu aliyetubu ambaye amesimama hapa, na ikiwa nimepata

neema machoni Pako, na tumeihubiri Injili pasipo kupatana, jinsi tu Neno linavyoifundisha, Nawe umethibitisha kwamba ni kweli kwa kututembelea usiku wa leo, Mungu, tusamehe kila dhambi, ondolea mbali kila baridi kutoka kwa watu hawa, na jalia Roho Mtakatifu, katika nguvu za kufufuka kwake Kristo, ataingia katika kila moyo na kuichangamsha mioyo hiyo, ijaze, Bwana.

187 Sasa hivi jalia Pentekoste nyingine ishuke juu ya wasikilizaji hawa. Shetani ameshindwa. Uweza wa Mungu na uingie mioyoni, na kutakasa na kujaza kila moyo hapa katika uwezo wa Kiungu wa Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana. Ninatoa maombi haya Kwako, Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo, tujalie, Baba. Jalia neema Yako, iturehemu, sisi, kukusanyika kwetu usiku wa leo na baraka zetu pamoja na Wewe, Bwana, katika mahali pa Mbinguni. Tujalie, katika Jina la Yesu.

188 Wote wanaoamini sasa, kwa moyo wako wote, kwamba Mungu anakusamehe, nawe unaahidi ya kwamba, kwa neema ya Mungu, Mbele za Malaika huyu, Roho Mtakatifu, aliye hapa sasa, unaahidi, tangu usiku huu na kuendelea, utamwishia Yeye, utaomba zaidi, utajitolea, utafunga, utafanya kila kitu katika uwezo wako, kwa neema ya Mungu, kumwishia Yeye, inueni mikono yenu na kumsifu. Sasa, semeni, “Asante, Bwana, kwa kunipa imani hii ya kuiamini.” Mungu awabariki. Amina.

62-0728 Mungu Anayo Njia Iliyoandaliwa
Curling Arena
Victoria, British Columbia Canada

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org